

MaarifaMtandaoni.com | SamaritanLaymenMinistries.Org

MAISHA YALIYOTAKASWA

Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

Enendeni Mtandaoni Kote

Shukurani:

Kwa Mwenyezi Mungu,
Watafsiri, Waombezi,
Wahariri, Wahakiki Washauri,
Wataalamu wa Teknolojia, na Watia M
oyo Wote

1.Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani
2.Nhandi Masunga, Mpwapwa, Tanzania
3. Sharon Ondieki, Nairobi, Kenya
4. E. Masige-Nairobi, Kenya
5. Daudi na Denis Masaka-Carolina, Marekani
6. Daniel Masaka-Kisii, Kenya
7. Sandra Barron-Carolina, Marekani
8.Judi Mmari Mugane-Boston, Marekani
9. John Mugane-Boston, Marekani

Neno kwa Msomaji

Chini ya kichwa cha jumla cha **“Kutakaswa,”** mfululizo wa makala zilizoandikwa na Ellen G. White ulitokea katika matoleo ya awali ya *Review and Herald* ya mwaka 1881. Akiandika kutokana na uzoefu wa kina katika mambo ya Mungu, na akiwa na akili na moyo vilivyoangazwa na Roho Mtakatifu, Bi. White alichunguza kwa uangalifu vipengele vya **utakaso wa**

Kweli na kuvilinganisha na nadharia mbalimbali zisizo sahihi, lakini zilizo maarufu, kuhusu jambo hilo. **{SLsw 5.1}**

Makala hizi zilichapishwa pamoja katika mfumo wa kijitabu mnamo Januari 1889. Kikiwa na kichwa **Bible Sanctification** (*Kutakaswa kwa Kibiblia*), kijitabu hicho kilitolewa kama namba ya kwanza ya **Bible Students' Library** (*Maktaba ya Wanafunzi wa Biblia*). **{SLsw 5.2}**

Mwaka 1937, pamoja na kuongezwa kwa fungu moja kutoka katika *Prophets and Kings* (*Manabii na Wafalme*), nyenzo hii ilichapishwa tena chini ya kichwa **The Sanctified Life** (*Maisha Yaliyotakaswa*), na hivyo kuunda juzuu hii ya sasa. Katika mfumo huu na kupitia matoleo mengi, kitabu hiki kidogo kimekuwa baraka kwa maelfu ya watu na kimeyaboresha maisha yao. **{SLsw 5.3}**

Katika muundo mpya, lakini bila mabadiliko yoyote katika maudhui ya maandishi, kitabu hiki chenye kina cha kiroho na kilichodumu kwa muda mrefu kinachapishwa tena ili kisambazwe kwa upana zaidi. Kwa urahisi wa msomaji, faharasa za Maandiko na za mada zimeongezwa. **{SL 5.4}**

Chapisho hili la sasa linatambuliwa katika **Comprehensive Index to the Writings of Ellen G. White** (*Faharasa Kamili ya Maandishi ya Ellen G. White*) na katika marejeo ya kazi hii yanayopatikana katika **The Seventh-day Adventist Bible Commentary** (*Ufafanuzi wa Biblia wa Waadventista wa Sabato*). **{SLsw 5.5}**

Wadhamini wa Ellen G. White Publications

Silver Spring, Maryland

Machi, 2006.

Mwongozo wa Kujifunza wa Maisha Yaliyotakaswa

Mwongozo kamili wa sura baada ya sura, wenye maswali ya kukusaidia kusoma na kuelewa kitabu hiki. **{SLsw 5.6}**

YALIYOMO

SURA YA 1—NADHARIA ZA KWELI NA ZA UONGO ZIKITOFAUTISHWA……4

SURA YA 2— KANUNI ZA KIASI ZA DANIELI ……..…...……11

SURA YA 3— KUDHIBITI TAMAA ZA CHAKULA NA TAMAA ZA MWILI ……16

SURA YA 4— TANURU LA MOTO ……..…… ……22

SURA YA 5— DANIELI KATIKA TUNDU LA SIMBA ……...28

SURA YA 6— MAOMBI YA DANIELI …… ……..31

SURA YA 7— TABIA YA YOHANA …… ……...36

SURA YA 8— HUDUMA YA YOHANA …… …….41

SURA YA 9— YOHANA UHAMISHONI ……. …….47

SURA YA 10— TABIA YA KIKRISTO ……. …….55

SURA YA 11— UPENDELEO WA MKRISTO……..……...61

SURA YA 1—NADHARIA ZA KWELI NA ZA UONGO ZIKITOFAUTISHWA

Utakaso unaofafanuliwa katika Maandiko Matakatifu unahusu nafsi yote—roho, nafsi, na mwili. Hapa tunaona maana ya kweli ya kujiweka wakfu kikamilifu. Paulo anaomba kwamba kanisa la Thesalonike lifurahie baraka hii kuu: ***"Mungu wa amani Mwenyewe awatakase***

kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja Kwake Bwana wetu Yesu Kristo." (1 Wathesalonike 5:23). **{SLsw 7.1}**

Katika ulimwengu wa kidini, kuna nadharia ya utakaso ambayo yenyewe ni ya uongo na ambayo ushawishi wake ni hatari. Katika hali nyingi, wale wanaodai kuwa wametakaswa hawana utakaso wa Kweli. Utakaso wao unajumuisha maneno tu, kaida na ibada za kujitungia mwenyewe katika mawazo yao ya kianadamu, na wala hazitoki kwa Mungu. Wale ambao kwa kweli wanatafuta kukamilisha tabia ya Kikristo hawatawahi kujidanganya wenyewe kwamba hawana dhambi. Maisha yao yanaweza kuwa yasiyo na lawama; wanaweza kuwa wawakilishi hai wa ile Kweli waliyoikubali; lakini kadiri wanavyozoeza akili zao kutafakari juu ya tabia ya Kristo, na kadiri wanavyoukaribia zaidi Mfano Wake wa Kiungu, ndivyo watakavyozidi kutambua kwa uwazi ukamilifu Wake usio na doa, na ndivyo watakavyohisi kwa undani zaidi mapungufu yao wenyewe. **{SLsw 7.2}**

Watu wanapodai kwamba wametakaswa, wanatoa ushahidi wa kutosha kwamba wako mbali na kuwa watakatifu. Wanashindwa kuona udhaifu wao wenyewe

na hali yao ya uhitaji. Wanajiona kuwa wanaakisi Mfano wa Kristo, kwa sababu hawana ujuzi wa Kweli kumhusu Yeye. Kadiri umbali ulivyo mkubwa kati yao na Mwokozi wao, ndivyo wanavyojiona kuwa ni wenye haki zaidi machoni pao wenyewe. **{SLsw 8.1}**

Tunapomtazama Yesu kwa moyo wa toba na kwa imani yenye unyenyekevu—Yeye ambaye dhambi zetu zilimchoma na huzuni zetu zikamlemea—tunaweza kujifunza kutembea katika nyayo Zake. Kwa kumtazama Yeye, tunabadilishwa kuwa mfano Wake wa Kiungu. Na kazi hii inapokuwa imetimizwa ndani yetu, hatutadai haki yoyote inayotokana na sisi wenyewe, bali tutamtukuza Yesu Kristo, huku tukizikabidhi nafsi zetu zisizo na msaada katika sifa, haki na stahiki Zake. **{SLsw 8.2}**

Kujihesabia Haki Kumekatazwa

Mwokozi wetu alikemea daima mtu kujiona kuwa ni mwenye haki. Aliwafundisha wanafunzi Wake kwamba kiwango cha juu kabisa cha dini ni kile kinachojidhihirisha kwa utulivu na bila kujionyesha. Aliwaonya wafanye matendo yao ya huruma kwa utulivu-

kimya-kimya; si kwa ajili ya kujionyesha, wala ili kusifiwa au kuheshimiwa na wanadamu, bali kwa ajili ya utukufu wa Mungu, wakitarajia thawabu yao katika maisha yajayo. Ikiwa wangetenda mema ili wasifiwe na wanadamu, Baba yao aliye mbinguni asingewapa thawabu yoyote. **{SLsw 8.3}**

Wafuasi wa Kristo walifundishwa wasisali kwa kusudi la kusikiwa na wanadamu. ***"Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba Yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi."*** (Mathayo 6:6). Maneno kama haya yaliyotoka katika kinywa cha Kristo yanaonyesha kwamba Yeye Hakukubaliana na aina ile ya kicho na uchaji wa Mungu iliyokuwa imeenea sana miongoni mwa Mafarisayo. Mafundisho Yake aliyotoa mlimani yanaonyesha kwamba matendo ya ukarimu hufikia hadhi ya juu, na matendo ya ibada ya kidini hutoa harufu nzuri yenye thamani kubwa zaidi yanapofanywa bila kujionyesha, kwa toba na unyenyekevu. Nia safi hutakasa tendo**. {SLsw 8.4}**

Utakaso wa Kweli ni kulingana kikamilifu na mapenzi ya Mungu. Mawazo na hisia za uasi hushindwa, na sauti ya Yesu huamsha maisha mapya, ambayo huenea

na kurindima katika nafsi yote. Wale ambao wametakaswa kwa kweli hawataifanya nia au oni lao wenyewe kuwa kipimo cha yaliyo mema na yaliyo mabaya. Hawana ushupavu wa kupita kiasi wala kujihesabia haki; bali hujichunguza wenyewe kwa wivu mtakatifu, wakihofia daima kwamba, kwa kuwa wameachiwa ahadi, huenda wakakosa kutimiza masharti ambayo ahadi hizo zimejengwa juu yake. **{SLsw 9.1}**

Kuweka Hisia Mahali pa Mantiki

Wengi wanaodai kuwa wametakaswa hawajui kabisa kazi ya neema moyoni. Wanapojaribiwa na kupimwa, huonekana kuwa kama yule Mfarisayo aliyejiona kuwa mwenye haki. Hawatakubali kupingwa. Wanaweka kando mantiki/busara na uamuzi wa hekima, na hutegemea kabisa hisia zao, wakijenga madai yao ya utakaso juu ya hisia ambazo wakati fulani walizipitia. Wao ni wakaidi na wapotovu katika kusisitiza madai yao ya kudumu ya utakatifu, wakitumia maneno mengi, lakini bila kuzaa matunda ya thamani kuwa ushahidi wa madai yao. Watu hawa wanaodai kuwa wametakaswa hawajidanganyi nafsi zao wenyewe tu kwa madai yao hayo, bali pia wanatoa ushawishi unaowapotosha wengi wanaotamani kwa dhati kupatana na mapenzi ya Mungu. Huenda ukawasikia

wakirudia tena na tena: “Mungu ananiongoza mimi! Mungu ananifundisha mimi! Mimi ninaishi bila dhambi!” Wengi wanaokutana na roho hii huhisi uwepo wa jambo fulani lenye giza na la fumbo ambalo hawawezi kulielewa. Lakini jambo hilo ni kinyume kabisa na Kristo, ambaye Ndiye Kielelezo pekee cha Kweli. **{SLsw 9.2}**

Utakaso wa Kibiblia haujumuishi hisia kali. Hapa ndipo wengi wanapoongozwa katika kosa. Wanafanya hisia zao kuwa kipimo. Wanapojisikia wamechangamka au wenye furaha, hudai kwamba wametakaswa. Hisia za furaha au kutokuwepo kwa furaha si ushahidi kwamba mtu ametakaswa au kwamba hajatakaswa. Hakuna kitu kama utakaso wa papo kwa papo. Utakaso wa Kweli ni kazi ya kila siku, inayoendelea maadamu maisha yanaendelea. Wale wanaopambana na majaribu ya kila siku, wakishinda mielekeo yao wenyewe ya dhambi, na kutafuta utakatifu wa moyo na maisha, hawajisifu kwa madai ya utakatifu. Wanakuwa na njaa na kiu ya haki. Dhambi huonekana kwao kuwa ni dhambi mbaya sana. **{SLsw 10.1}**

Kuna watu wanaodai kuwa wametakaswa ambao, kama ndugu zao, wanakiri kweli; na huenda ikawa vigumu kutofautisha kati yao, lakini tofauti hiyo ipo hata

hivyo. Ushuhuda wa wale wanaodai kuwa wamefikia uzoefu huo wa hali ya juu utamfanya Roho mpole wa Kristo ajiondoe katika mkutano, na kuwaachia waliopo humo ushawishi wa kuwafanya wapoe kiroho; lakini kama kweli wangekuwa wanaishi bila dhambi, uwepo wao wenyewe ungeleta malaika watakatifu katika kusanyiko, na maneno yao kwa kweli yangekuwa ***"Neno linenwalo wakati wa kufaa, ambalo ni kama machungwa katika vyano vya fedha."*** (Mithali 25:11). **{SLsw 10.2}**

Wakati wa Kujaribiwa

Katika majira ya kiangazi, tunapotazama miti ya msitu wa mbali, ikiwa yote imefunikwa na vazi zuri la kijani kibichi, huenda tusiweze kutofautisha kati ya miti ya kijani kibichi daima kama ile ya Krismasi na miti mingine. Lakini majira ya baridi na theluji yanapokaribia, na mfalme wa baridi kali yenye barafu za juujuu anapoifunika kwa kumbatio lake la theluji, akiinyang'anya miti mingine majani yake mazuri, miti ya kijani kibichi daima hutambulika kwa urahisi. Ndivyo itakavyokuwa kwa wote wanaotembea kwa unyenyekevu, wasiojitumaini wenyewe, bali wanaushikilia kwa kutetemeka mkono wa Kristo. Wakati wale wanaojiamini

wenyewe na kutegemea ukamilifu wa tabia zao wanapopoteza vazi lao la uongo la haki wanapokabiliwa na dhoruba za majaribu, wenye haki wa Kweli, wanaompenda na kumcha Mungu kwa unyofu, huvaa vazi la haki ya Kristo katika mafanikio na katika taabu vilevile. **{SLsw 11.1}**

Kujikana nafsi, kujitoa mhanga, ukarimu, wema, upendo, uvumilivu, uthabiti, na imani ya Kikristo, ni matunda ya kila siku yanayozalishwa na wale walio katika uhusiano wa kweli na Mungu. Matendo yao huenda yasitangazwe kwa ulimwengu, lakini wao wenyewe kila siku wanapambana na uovu na kupata ushindi wa thamani juu ya majaribu na makosa. Nadhiri za dhati hufanywa upya na kutimizwa kwa nguvu inayopatikana kupitia maombi ya bidii na kukesha daima. Mtu shupavu mwenye hamasa haoni mapambano ya wafanyakazi hawa watulivu; lakini jicho la Yeye aonaye siri za moyo huona na kukubali kwa furaha kila jitihada inayofanywa kwa unyenyekevu na upole. Ni wakati wa kujaribiwa unaofunua dhahabu safi ya upendo na imani katika tabia. Majaribu na mashaka yanapolipata kanisa, ndipo bidii thabiti na mapenzi ya dhati ya wafuasi wa Kweli wa Kristo yanapodhihirika. **{SLsw 11.2}**

Tunahuzunika kuwaona Wakristo wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wakipotoshwa na nadharia ya uongo na yenye kupotosha kwamba wao ni wakamilifu, kwa sababu ni vigumu sana kuwasaidia watambue udanganyifu huo na kuwaongoza katika njia iliyo sahihi. Wamejitahidi kuufanya mwonekano wa nje uwe mzuri na wenye kuvutia, huku pambo la ndani—yaani, upole na unyenyekevu wa Kristo—likikosekana. Wakati wa kujaribiwa utawajia wote, ambapo matumaini ya wengi ambao kwa miaka mingi wamejiona kuwa salama yataonekana kuwa hayakuwa na msingi. Wanapowekwa katika nafasi mpya na chini ya hali mbalimbali, baadhi ya wale ambao walionekana kuwa nguzo katika nyumba ya Mungu hufunua kwamba chini ya rangi na varnishi ya kung'arisha, kulikuwa na mbao zilizooza tu. Lakini wale walio wanyenyekevu moyoni, ambao kila siku wamehisi umuhimu wa kuzikaza nafsi zao kwenye Mwamba wa milele, watasimama bila kutikisika katikati ya dhoruba za majaribu, kwa sababu hawakujitumaini wenyewe. ***"Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye muhuri hii, Bwana awajua walio Wake. Na tena, Kila alitajaye Jina la Bwana na auache uovu."*** (2 Timotheo 2:19). **{SLsw 12.1}**

Kuzaa Matunda kwa Kawaida

Wale wanaojitahidi kuvutia watu waangalie matendo yao mema, wakizungumza daima kuhusu hali yao ya kutokuwa na dhambi na kujitahidi kuyafanya mafanikio yao ya kidini yaonekane wazi, kwa kufanya hivyo wanajidanganya tu nafsi zao wenyewe. Mtu mwenye afya njema, anayeweza kushughulikia shughuli za maisha na ambaye huenda kazini siku baada ya siku akiwa na uchangamfu na damu yenye afya ikitiririka katika mishipa yake, hamwelekezi kila mtu anayekutana naye kwenye hali njema ya mwili wake. Afya na nguvu ni hali za kawaida za maisha yake; kwa hiyo, huwa ni kama hajitambui kwamba anafurahia baraka hiyo kubwa. **{SLsw 12.2}**

Ndivyo ilivyo kwa mtu mwenye haki wa kweli. Yeye hajitambui kuwa mwema na mcha Mungu. Kanuni za kidini zimekuwa msingi wa maisha na mwenendo wake, na kwake ni jambo la kawaida kabisa kuzaa matunda ya Roho, kama ilivyo kawaida kwa mtini kuzaa tini au mti wa waridi kutoa maua ya waridi. Asili yake imejaa kabisa upendo kwa Mungu na kwa wanadamu wenzake, hivi kwamba hutenda matendo ya Kristo kwa moyo wa hiari. **{SLsw 13.1}**

Wote walio ndani ya eneo la ushawishi wake, huona uzuri na manukato ya maisha yake ya Kikristo, naye mwenyewe hatambui jambo hilo, kwa sababu linaafikiana na mazoea na mielekeo yake. Huomba nuru ya Mungu, na hupenda kutembea katika nuru hiyo. Ni chakula na kinywaji chake kufanya mapenzi ya Baba yake wa mbinguni. Maisha yake yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu; hata hivyo, hajisifu kwa jambo hili, wala haonekani kulifahamu. Mungu huwafurahia wanyenyekevu na wapole wanaofuata kwa karibu nyayo za Bwana wao. Malaika huvutiwa nao, na hupenda kukaa karibu na njia yao. Wanaweza kupuuzwa na wengine kwamba hawastahili kuangaliwa au kushugulikiwa na wale wanaodai kuwa wamefikia viwango vya juu vya kiroho na wanaopenda kuyafanya matendo yao mema yaonekane wazi, lakini malaika wa mbinguni huinama kwa upendo juu yao na huwa kama ukuta wa moto unaowazunguka. **{SLsw 13.2}**

Kwa Nini Kristo Alikataliwa

Mwokozi wetu alikuwa nuru ya ulimwengu, lakini ulimwengu haukumjua. Alikuwa akijishughulisha daima na matendo ya rehema, akiangaza njia ya wote; hata hivyo, hakuwataka wale aliokutana nao watazame wema Wake

usio na kifani, kujikana Kwake, kujitoa Kwake mhanga, na ukarimu Wake. Wayahudi hawakuvutiwa na maisha ya namna hiyo. Waliona dini Yake kuwa haina thamani, kwa sababu haikupatana na kiwango chao cha uchaji wa Mungu. Waliamua kwamba Kristo hakuwa na roho wala tabia ya kidini; kwa maana dini yao ilijumuisha kujionyesha/maonyesho, kusali hadharani, na kufanya matendo ya hisani kwa kusudi la kujionyesha. Walijivunia na kutangaza matendo yao mema, kama wafanyavyo wale wanaodai kuwa wametakaswa. Walitaka kila mtu ajue kwamba wao hawana dhambi. Lakini maisha yote ya Kristo yalikuwa kinyume kabisa na hayo. Yeye Hakutafuta faida wala heshima. Matendo Yake ya ajabu ya uponyaji yalifanywa kwa utulivu mkubwa kadiri ilivyowezekana, ingawa hakuweza kuzuia shauku ya wale waliopokea baraka Zake kuu. Unyenyekevu na upole vilitawala katika maisha Yake. Na ilikuwa kwa sababu ya mwenendo Wake wa unyenyekevu na tabia Yake ya kutokujionyesha, kujifanya, ambavyo vilitofautiana sana na vyao wenyewe, kwamba Mafarisayo hawakumkubali. **{SLsw 14.1}**

Upole—Tunda la Roho

Tunda la thamani zaidi la utakaso ni neema ya upole. Neema hii inapotawala moyoni, mwenendo wa mtu huumbwa chini ya ushawishi wake. Kuna kumngoja Mungu daima na kujitiisha/kujisalimisha kwa mapenzi Yake. Ufahamu hushika kila Kweli ya Mungu, na mapenzi huinama mbele ya kila amri ya Mungu, bila mashaka wala kunung'unika. Upole wa kweli huulainisha na kuutuliza moyo, na kuifanya akili iwe tayari kulipokea Neno lililopandwa moyoni. Huleta mawazo katika utiifu kwa Yesu Kristo. Hufungua moyo kwa Neno la Mungu, kama moyo wa Lidia ulivyofunguliwa. Hutuweka pamoja na Mariamu, kama wanafunzi, miguuni pa Yesu (Matendo 16). ***"Wenye upole atawaongoza katika hukumu, Wenye upole atawafundisha njia Yake."*** (Zaburi 25:9). **{SLsw 14.2}**

Lugha ya wenye unyenyekevu na upole si lugha ya kujisifu kamwe. Kama mtoto Samweli, wao huomba, ***"Nena, Bwana; kwa kuwa mtumishi wako anasikia"*** (1 Samweli 3:9). Yoshua alipowekwa katika nafasi ya juu kabisa ya heshima, akiwa jemadari wa Israeli, aliwakabili bila woga maadui wote wa Mungu. Moyo wake ulijawa na mawazo matukufu kuhusu utume wake mkuu. Hata hivyo, alipojulishwa kwamba ujumbe kutoka Mbinguni ulikuwa unamjia, alijiweka katika hali ya mtoto mdogo,

tayari kuelekezwa. ***"Bwana wangu aniambia nini mimi mtumishi Wake?"*** (Yoshua 5:14) ndilo lilikuwa jibu lake. Maneno ya kwanza ya Paulo baada ya Kristo kufunuliwa Kwake yalikuwa, ***"Bwana, wataka nifanye nini?"*** (Matendo 9:6). **{SLsw 15.1}**

Upole katika shule ya Kristo ni mojawapo ya matunda dhahiri ya Roho. Ni neema inayofanyizwa na Roho Mtakatifu akiwa Mtakasaji, na humwezesha mwenye neema hiyo kudhibiti daima hasira ya ghafla na ya msukumo. Neema ya upole inapothaminiwa na wale ambao kwa asili yao wana tabia ya ukali/ugwadu au ya pupa, watajitahidi kwa dhati sana kuitawala tabia yao hiyo isiyopendeza. Kila siku watapata kujitawala zaidi, mpaka kile kisichopendeza na kisichofanana na Yesu kitakaposhindwa. Watazidi kufanana na Kielelezo cha Kiungu, mpaka waweze kutii agizo lililoongozwa na Roho, lisemalo: ***"Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika;"*** (Yakobo 1:19). **{SLsw 15.2}**

Mtu anapodai kuwa ametakaswa, lakini kwa maneno na matendo yake anaweza kufananishwa na chemchemi chafu inayotoa maji machungu, tunaweza kusema kwa hakika kwamba mtu huyo amedanganyika. Anahitaji

kujifunza hata hatua rahisi za mwanzo, yaani alfabeti ya mambo yanayounda maisha ya Mkristo. Baadhi ya wale wanaodai kuwa watumishi wa Kristo wamelea kwa muda mrefu sana roho ya kutokuwa na fadhili, hivi kwamba wanaonekana kuupenda ushawishi huo usio mtakatifu na kufurahia kusema maneno yanayokera na kukasirisha. Watu hawa lazima waongoke kabla Kristo hajawakiri kuwa watoto Wake. **{SLsw 16.1}**

Upole na unyenyekevu ni pambo la ndani, ambalo Mungu huliona kuwa la thamani kubwa. Mtume analizungumzia kuwa bora na lenye thamani zaidi kuliko dhahabu, lulu, au mavazi ya gharama kubwa. Ingawa pambo la nje hupamba mwili wa kufa tu, pambo la upole hupamba nafsi na kumunganisha mwanadamu mwenye mipaka na Mungu asiye na mipaka. Hili ndilo pambo alilolichagua Mungu Mwenyewe. Yeye aliyeziremba mbingu kwa mianga ya mbinguni, kwa Roho Huyo Huyo ameahidi kwamba ***"atawapamba wenye upole kwa wokovu"*** (Zaburi 149:4). Malaika wa mbinguni watawaona kuwa waliopambwa vizuri zaidi wale wanaomvaa Bwana Yesu Kristo na kutembea pamoja Naye katika upole na unyenyekevu wa moyo. **{SLsw 16.2}**

Kuna viwango vya juu vya kufikiwa kwa Mkristo. Anaweza daima kupanda na kufikia viwango vya juu zaidi. Yohana alikuwa na mtazamo wa juu kuhusu upendeleo wa kuwa Mkristo. Anasema, ***"Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu"*** (1 Yohana 3:1). Haiwezekani kwa mwanadamu kufikia hadhi iliyo juu zaidi kuliko ile inayodokezwa hapa. Mwanadamu amepewa fursa ya kuwa mrithi wa Mungu na mrithi pamoja na Kristo. Kwa wale ambao wameinuliwa hivyo, hufunuliwa utajiri wa Kristo usiopimika, ambao una thamani mara elfu zaidi kuliko mali ya ulimwengu. Hivyo, kwa njia ya stahiki na sifa za Yesu Kristo, mwanadamu mwenye mipaka huinuliwa na kuingia katika ushirika na Mungu na Mwana Wake mpendwa. **{SLsw 16.3}**

SURA YA 2—KANUNI ZA KIASI ZA DANIELI

Nabii Danieli alikuwa mtu mashuhuri sana. Alikuwa mfano anang'aa kwa ubora wa kile ambacho wanadamu wanaweza kuwa wanapounganishwa na Mungu wa hekima. Simulizi fupi la maisha ya mtu huyu mtakatifu wa Mungu limehifadhiwa kwa ajili ya kuwatia moyo wale ambao baadaye wangeitwa kustahimili majaribu na vishawishi. **{SLsw 18.1}**

Watu wa Israeli, pamoja na mfalme wao, wakuu wao, na makuhani wao, walipopelekwa utumwani, vijana wanne miongoni mwao walichaguliwa kutumika katika ikulu ya mfalme wa Babeli. Mmoja wao alikuwa Danieli, ambaye tangu mapema alionyesha dalili za uwezo wa pekee ambao ulidhihirika zaidi katika miaka iliyofuata. Vijana hawa wote walikuwa wa uzao wa kifalme, na wanaelezwa kuwa ***"vijana wasio na mawaa, wazuri wa uso, wajuzi wa hekima, werevu kwa sababu ya maarifa yao, wenye kufahamu elimu, watakaoweza kusimama katika jumba la mfalme;"*** (Danieli 1:4). Mfalme Nebukadneza alipotambua vipawa bora vya vijana hawa waliochukuliwa kama mateka, aliamua kuwaandaa ili washike nafasi muhimu katika ufalme wake. Ili waweze kuhitimu kikamilifu kwa ajili ya maisha yao ya ikuluni, kulingana na desturi za Mashariki, walipaswa kufundishwa lugha ya Wakaldayo na kufanyiwa mafunzo ya kina ya kuzoezwa na kuimarishwa mwili na akili kwa muda wa miaka mitatu. **{SLsw 18.2}**

Vijana waliokuwa katika shule hii ya mafunzo hawakupaswa tu kuruhusiwa kuingia katika jumba la kifalme, bali iliamuliwa pia kwamba wale nyama na kunywa divai iliyotoka katika meza ya mfalme. Katika mambo haya yote, mfalme alifikiri kwamba hakuwa tu

akiwapa heshima kubwa, bali pia alikuwa akihakikisha kwamba wanapata maendeleo bora zaidi ya kimwili na kiakili ambayo yangeweza kufikiwa. **{SLsw 19.1}**

Kukabiliana na Jaribu au Mtihani

Miongoni mwa vyakula vilivyowekwa mbele ya mfalme kulikuwa na nyama ya nguruwe na nyama nyingine zilizobainishwa kuwa najisi kwa mujibu wa sheria ya Musa, ambazo Waebrania walikuwa wamekatazwa waziwazi kula. Hapa Danieli alikabiliwa na jaribu kubwa. Je, angeshikilia mafundisho ya baba zake kuhusu vyakula na vinywaji, na hivyo kumchukiza mfalme, na huenda akapoteza si tu nafasi yake bali pia maisha yake? Au angepuuza amri ya Bwana na kuendelea kupata kibali cha mfalme, na hivyo kujipatia faida kubwa za kiakili pamoja na kujikomba/kujidanganya katika kujipatia matarajio mazuri zaidi ya kidunia? **{SLsw 19.2}**

Danieli hakusita kwa muda mrefu. Aliakusudia kusimama imara katika uadilifu wake, bila kujali matokeo yangekuwa nini. ***"Aliazimia moyoni mwake kwamba hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa"*** (Danieli 1:8). **{SLsw 19.3}**

Si Mfinyu kwa akili Wala Mwenye Ushupavu wa Kupita Kiasi

Leo kuna wengi miongoni mwa Wakristo wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo ambao wangeamua kwamba Danieli alikuwa mwenye kushikilia mambo kwa kupitiliza kiasi, na wangemwona kuwa mtu mwenye akili finyu na mwenye ushupavu wa kupita kiasi. Wanaona kwamba suala la kula na kunywa ni jambo dogo sana kiasi kwamba haliihitaji msimamo wa kuazimia kwa uthabiti kama huo—msimamo ambao ungeweza kuhusisha kujitoa mhanga kwa kila faida ya kidunia. Lakini wale wanaofikiri hivyo watagundua siku ya hukumu kwamba waligeuka kutoka katika matakwa ya wazi ya Mungu na kuweka maoni yao wenyewe kuwa kipimo cha mema na mabaya. Watagundua kwamba jambo lililoonekana kwao kuwa lisilo na umuhimu, halikuonekana hivyo na Mungu. Matakwa Yake yanapaswa kutiiwa kwa heshima takatifu. Wale wanaokubali na kutii mojawapo ya amri Zake kwa sababu tu ni mtelekemko kufanya hivyo, huku wakikataa nyingine kwa sababu kuitii kungehitaji kujitoa mhanga, hushusha kiwango cha mema na, kwa mfano wao, huwafanya wengine kuichukulia kwa wepesi sheria takatifu ya Mungu. ***"Bwana asema hivi"*** ndiyo inapaswa kuwa kanuni yetu katika mambo yote. **{SLsw 19.4}**

Tabia Isiyo na Lawama

Danieli alikabiliwa na vishawishi vikali zaidi vinavyoweza kuwakabili vijana wa leo; hata hivyo, alibaki kuwa mwaminifu kwa mafundisho ya kidini aliyoyapokea tangu utotoni. Alizungukwa na ushawishi uliokusudiwa kuwapotosha wale ambao wangesitasita kati ya kanuni na mielekeo yao; hata hivyo, Neno la Mungu linamweka mbele yetu kuwa mtu mwenye tabia isiyo na lawama. Danieli hakuthubutu kutegemea nguvu zake mwenyewe za kimaadili. Maombi yalikuwa hitaji kwake. Alimfanya Mungu kuwa nguvu zake, na kumcha Mungu kulikuwa daima mbele yake katika shughuli zote za maisha yake. **{SLsw 20.1}**

Danieli alikuwa na neema ya upole wa kweli/dhati. Alikuwa mwaminifu, thabiti, na mwenye heshima. Alitafuta kuishi kwa amani na wote, huku akiwa asiyeyumbishwa kama mwerezi mrefu kila mahali ambapo kanuni zilihusika. Katika kila jambo ambalo halikugongana na uaminifu wake kwa Mungu, alikuwa mwenye heshima na mtiifu kwa wale waliokuwa na mamlaka juu yake; lakini alikuwa na ufahamu wa juu sana wa madai ya Mungu kiasi kwamba, matakwa ya watawala wa kidunia yaliwekwa chini ya hayo ya Bwana. Hakuruhusu jambo lolote la kujinufaisha limshawishi kuacha wajibu wake. **{SLsw 20.2}**

Tabia ya Danieli imewekwa mbele ya ulimwengu kama mfano wa kuvutia wa kile ambacho neema ya Mungu inaweza kuwafanya wanadamu walioanguka kwa asili na kuharibiwa na dhambi. Kumbukumbu ya maisha yake ya uadilifu ya kujikana nafsi ni faraja kwa wanadamu wenzetu. Kutokana na huu, tunaweza kupata nguvu za kupinga kwa ujasiri majaribu na kusimama imara kwa ajili ya yaliyo mema, kwa uthabiti na katika neema ya upole, katikati ya majaribu makali zaidi. **{SLsw 21.1}**

Kibali cha Mungu Kilikuwa Cha Thamani Kuliko Maisha

Danieli angeweza kupata kisingizio kinachoeleweka cha kuacha mazoea yake ya kiasi, lakini kibali cha Mungu kilikuwa cha thamani zaidi kwake kuliko kibali cha mtawala mwenye nguvu zaidi wa kidunia—naam, kilikuwa cha thamani zaidi hata kuliko maisha yenyewe. Baada ya kupata kibali cha Melzari kwa mwenendo wake wa heshima, Danieli aliomba kwamba yeye na wenzake wasile nyama ya mfalme wala kunywa divai yake. Melzari aliogopa kwamba akikubali ombi hilo, angeweza kumchukiza mfalme na hivyo kuhatarisha maisha yake mwenyewe. Kama watu wengi wa siku hizi, alifikiri

kwamba chakula cha kiasi kingewafanya vijana hawa waonekane wamepauka na wagonjwa, na kukosa nguvu za misuli, ilhali vyakula vya anasa kutoka katika meza ya mfalme vingewafanya wawe na rangi nzuri na wenye kuvutia, na vingechochea shughuli za mwili na akili. **{SLsw 21.2}**

Danieli aliomba kwamba jambo hilo liamuliwe kwa jaribio la siku kumi—katika kipindi hicho kifupi vijana Waebrania waruhusiwe kula chakula sahili, huku wenzao wakila vyakula vitamu vya mfalme. Hatimaye ombi hilo lilikubaliwa, na ndipo Danieli alihakikishiwa kwamba ombi lake lilikuwa limekubaliwa. Ingawa alikuwa kijana tu, alikuwa ameona madhara ya divai na maisha ya anasa kwa afya ya mwili na akili. **{SLsw 22.1}**

Mungu Anamtetea Mtumishi Wake

Mwishoni mwa siku hizo kumi, matokeo yalikuwa kinyume kabisa na matarajio ya Melzari. Si katika mwonekano wa nje pekee, bali pia katika shughuli za mwili na uchangamfu wa akili, wale waliokuwa na mazoea ya kiasi walionyesha ubora wa wazi kuliko wenzao waliokuwa wamejiruhusu kutawaliwa na tamaa ya chakula. Kutokana na jaribio hilo, Danieli na wenzake waliruhusiwa kuendelea na chakula chao sahili katika

kipindi chote cha mafunzo yao kwa ajili ya majukumu ya ufalme. **{SLsw 22.2}**

Bwana aliutazama kwa kibali uthabiti wao na kujikana kwao nafsi, na baraka Yake ilikuwa pamoja nao. ***"Basi, kwa habari za hao vijana wanne, Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote, na ndoto."*** (Danieli 1:17). Miaka hiyo mitatu ya mafunzo ilipokwisha, na uwezo na maarifa yao yalipojaribiwa na mfalme, ***"miongoni mwao wote hawakuonekana waliokuwa kama Danielii, na Hanania, na Mishaeli, na Azaria; kwa hiyo wakasimama mbele ya mfalme. Na katika kila jambo la hekima na ufahamu alilowauliza mfalme, akawaona kuwa walifaa mara kumi zaidi ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake."*** (mstari wa 20). **{SLsw 22.3}**

Kujitawala—Sharti la Utakaso

Maisha ya Danieli ni kielelezo kilichowekwa kwenye Maandishi kupitia uvuvio kuhusu kile kinachounda tabia iliyotakaswa. Yanatoa somo kwa wote, na hasa kwa vijana. Kutii kikamilifu matakwa ya Mungu kuna manufaa kwa afya ya mwili na akili. Ili kufikia kiwango cha juu kabisa cha mafanikio ya kimaadili na kiakili, ni

lazima kutafuta hekima na nguvu kutoka kwa Mungu na kuzingatia kwa ukamilifu kanuni za kiasi katika mazoea yote ya maisha. Katika uzoefu wa Danieli na wenzake tunaona mfano wa ushindi wa kanuni dhidi ya jaribu la kujiruhusu kutawaliwa na tamaa ya chakula. Unatuonyesha kwamba kwa kufuata kanuni za kidini, vijana wanaweza kushinda tamaa za mwili na kubaki waaminifu kwa matakwa ya Mungu, hata kama ingewagharimu kujitoa mhanga sana. **{SLsw 23.1}**

Ingekuwaje kama Danieli na wenzake wangekubaliana na maafisa hao wa kipagani na kukubali shinikizo la wakati huo, kwa kula na kunywa kama ilivyokuwa desturi ya Wababeli? Tukio hilo moja tu la kuacha kanuni lingedhoofisha utambuzi wao wa yaliyo mema na chuki yao dhidi ya yaliyo mabaya. Kujiruhusu kutawaliwa na tamaa ya chakula kungesababisha kupoteza nguvu za mwili, uwazi wa akili, na uwezo wa kiroho. Hatua moja mbaya huenda ingesababisha nyingine, mpaka uhusiano wao na Mbingu ulipokatika, wangetekwa na jaribu. **{SLsw 23.2}**

Mungu amesema, ***"Kwa maana wale wanaoniheshimu nitawaheshimu"*** (1 Samweli 2:30). Danieli alipomshikilia Mungu wake kwa imani

isiyotikisika, Roho ya nguvu ya kinabii ilikuja juu yake. Ingawa alifundishwa na wanadamu kuhusu majukumu ya maisha ya ikulu, alifundishwa na Mungu kusoma siri za nyakati zijazo na, kupitia mifano na mafumbo, kuvitangazia vizazi vijavyo mambo ya ajabu ambayo yangetokea katika siku za mwisho. **{SLsw 24.1}**

SURA YA 3—KUDHIBITI TAMAA ZA CHAKULA NA TAMAA ZA MWILI

"Ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho," ndivyo asemavyo mtume Petro (1 Petro 2:11). Wengi huona fungu hili kuwa ni onyo dhidi ya uasherati pekee, lakini lina maana pana zaidi. Linakataza kila kujiridhisha kwa tamaa ya chakula au ya mwili kunakodhuru. Mtu yeyote anayekiri kumcha Mungu asidharau afya ya mwili, wala asijidanganye kwamba kutokuwa na kiasi si dhambi na kwamba hakutaathiri hali yake ya kiroho. Kuna uhusiano wa karibu kati ya hali ya kimwili na hali ya kimaadili. Mazoea yoyote yasiyochangia afya hudhoofisha vipawa vya juu na bora zaidi. Mazoea mabaya ya kula na kunywa huongoza kwenye makosa katika mawazo na matendo. Kujiridhisha kwa tamaa ya chakula au kuendekeza ulafi, huimarisha mielekeo ya kinyama, na kuifanya itawale nguvu za akili na za kiroho. **{SLsw 25.1}**

Haiwezekani mtu yeyote kufurahia baraka ya utakaso wakati akiwa mbinafsi na mlafi. Wengi wanateseka kwa udhaifu na magonjwa kwa sababu ya mazoea mabaya ya kula na kunywa, ambayo yanakiuka sheria za maisha na afya na kuunyanyasa mwili. Wanadhoofisha viungo vyao vya mfumo wa umeng'enyaji wa chakula kwa kujiruhusu kutawaliwa na tamaa potovu ya chakula. Uwezo wa mwili wa mwanadamu wa kustahimili madhara yanayofanywa juu yake ni wa ajabu; lakini mazoea mabaya ya kudumu

ya kula na kunywa kupita kiasi yatadhoofisha kila utendaji wa mwili. Katika kujiridhisha kwa tamaa potovu ya chakula na tamaa za mwili, hata Wakristo wanaodai kuwa wacha Mungu huathiri utendaji wa asili wa mwili na kupunguza nguvu za kimwili, kiakili, na kimaadili na hata kuleta ulema wa namna fulani. Watu hawa walio dhaifu watafakari wangekuwa watu wa namna gani ikiwa wangeishi kwa kiasi na kuitunza afya badala ya kuitumia vibaya. **{SLsw 25.2}**

Si Kiwango Kisichowezekana

Paulo alipoandika, ***"Mungu wa amani Mwenyewe awatakase kabisa"*** (1 Wathesalonike 5:23), hakuwa akiwahimiza ndugu zake kulenga kiwango ambacho hawangeweza kukifikia; wala hakuomba wapewe baraka ambazo haikuwa mapenzi ya Mungu kuwapa. Alijua kwamba wote ambao wangekuwa wameandaliwa kukutana na Kristo kwa amani walipaswa kuwa na tabia safi na takatifu. ***"Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; bali nautesa mwili wangu na***

kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa." (1 Wakorintho 9:25-27). ***"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu."*** (1 Wakorintho 6:19, 20). **{SLsw 26.1}**

Sadaka Isiyo na Dosari

Tena mtume anawaandikia waamini, ***"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana."*** (Warumi 12:1). Waisraeli wa kale walipewa maagizo hususani kwamba mnyama yeyote mwenye dosari au ugonjwa asitolewe kuwa sadaka kwa Mungu. Wanyama waliokuwa wakamilifu kabisa ndio pekee waliopaswa kuchaguliwa kwa kusudi hili. Kupitia nabii Malaki, Bwana aliwakemea kwa ukali sana watu Wake kwa kuyaacha maagizo hayo. **{SLsw 27.1}**

"Mwana humheshimu baba yake, na mtumishi humcha bwana wake; basi, kama Mimi ni baba yenu, heshima Yangu iko wapi? Na kama Mimi ni Bwana wenu, kicho Changu ki wapi? Bwana wa majeshi

awauliza ninyi, enyi makuhani, mnaolidharau jina Langu. Nanyi mwasema, Tumelidharau Jina Lako kwa jinsi gani? Mnatoa chakula kilichotiwa unajisi juu ya madhabahu yangu Nanyi mwasema, Sisi tumekutia unajisi kwa jinsi gani? Kwa sababu mwasema, Meza ya Bwana ni kitu cha kudharauliwa. Tena mtoapo sadaka aliye kipofu, si vibaya? Na mtoapo sadaka walio vilema na wagonjwa, si vibaya? Haya! Mtolee liwali wako; je! Atakuwa radhi nawe? Au atakukubali nafsi yako? Asema Bwana wa majeshi. Na sasa, nawasihi, ombeni fadhili za Mungu, ili atupe neema; ikiwa jambo hili limetoka katika mikono yenu; je! Atawakubali nafsi zenu? Asema Bwana wa majeshi. Laiti angekuwapo kwenu mtu mmoja wa kuifunga milango; msije mkawasha moto bure madhabahuni Pangu! Sina furaha kwenu, asema Bwana wa majeshi, wala sitakubali dhabihu yoyote mikononi mwenu. Kwa maana tokea maawio ya jua hata machweo yake Jina Langu ni kuu katika Mataifa; na katika kila mahali unatolewa uvumba na dhabihu safi kwa Jina Langu; maana Jina Langu ni kuu katika Mataifa, asema Bwana wa majeshi. Lakini ninyi mnalitia unajisi, kwa kuwa mwasema, Meza ya Bwana imetiwa unajisi; na matunda yake, yaani, nyama yake, hudharauliwa. Tena

mwasema, Tazama, jambo hili linatuchokesha namna gani! Nanyi mmelidharau, asema Bwana wa majeshi; nanyi mmeleta kitu kilichopatikana kwa udhalimu, na kilema, na kilicho kigonjwa; ndivyo mnavyoleta sadaka; je! Niikubali hii mikononi mwenu? Asema Bwana." (Malaki 1:6-13). **{SLsw 27.2}**

Ingawa maneno haya yalielekezwa kwa Israeli ya kale, yanafundisha somo kwa watu wa Mungu leo. Mtume anapowasihi ndugu zake watoe miili yao iwe ***"dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu,"*** anaweka wazi kanuni za utakaso wa kweli. Utakaso si nadharia tu, wala si hisia, wala si maneno ya kidini tu; bali ni kanuni iliyo hai na inayotenda kazi, inayoingia katika maisha ya kila siku. Inahitaji kwamba mazoea yetu ya kula, kunywa na kuvaa yawe ya namna inayolinda afya ya mwili, akili na maadili, ili tumtolee Bwana miili yetu, si sadaka iliyoharibiwa na mazoea mabaya, bali ***"dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu."*** **{SLsw 27.3}**

Vichocheo na Dawa za Kulevya (Stimulants and narcotics)

Onyo la mtume Petro la kujiepusha na tamaa za mwili ni onyo la moja kwa moja na lenye nguvu sana dhidi ya matumizi ya vichocheo na dawa za kulevya za

aina hii, kama vile chai, kahawa, tumbaku, pombe na morfini. Matumizi haya yanaweza kwa hakika kuhesabiwa miongoni mwa tamaa zinazokuwa na ushawishi mbaya juu ya tabia ya kimaadili. Kadiri mazoea haya yenye kudhuru yanavyoanza mapema, ndivyo yatakavyomfunga zaidi mwathirika wake katika utumwa wa tamaa, na ndivyo kwa hakika yatakavyoshusha kiwango cha kiroho. **{SLsw 28.1}**

Mafundisho ya Biblia yataacha mvuto dhaifu sana kwa wale ambao uwezo wao wa akili umepoozwa na kujiridhisha kwa tamaa zao wenyewe. Maelfu wako tayari kutoa kafara si katika afya na maisha yao tu, bali hata tumaini lao la mbinguni, badala ya kupigana dhidi ya tamaa zao wenyewe zilizopotoka. Mwanamke mmoja ambaye kwa miaka mingi alidai kuwa ametakaswa alisema kwamba ikiwa angelazimika kuacha kiko chake cha tumbaku au kuacha tumaini la mbinguni, angesema, “Kwaheri, mbingu; Siwezi kushinda/kuacha tamaa yangu ya kuvuta tumbaku kwa kiko.” Sanamu hii ilikuwa imepewa nafasi ya juu ndani ya nafsi yake, na hivyo alimwachia Yesu nafasi ya chini. Hata hivyo, mwanamke huyo alidai kwamba alikuwa wa Bwana kabisa! **{SLsw 28.2}**

Tamaa Zinazopigana na Nafsi

Popote walipo, wale ambao wametakaswa Kweli watainua kiwango cha maadili kwa kudumisha mazoea sahihi ya kimwili na, kama Danieli, kuwawekea wengine mfano wa kiasi na kujikana nafsi. Kila tamaa potovu huwa tamaa inayopigana na nafsi. Kila jambo linalopingana na sheria ya asili husababisha hali ya maradhi katika nafsi. Kujiridhisha kwa tamaa ya chakula au kuendekeza ulafi, husababisha tumbo kuwa na mmeng'enyo mbaya, ini kutofanya kazi kwa ufanisi, na akili kufunikwa na ukungu; na hivyo hupotosha tabia na roho ya mtu. Na nguvu hizi zilizodhoofishwa hutolewa kwa Mungu, ambaye alikataa kuzipokea sadaka isipokuwa ziwe bila dosari! Ni wajibu wetu kuleta tamaa zetu za chakula na mazoea yetu ya maisha yapatane na sheria ya asili. Ikiwa miili inayotolewa juu ya madhabahu ya Kristo ingechunguzwa kwa uchunguzi wa makini kama ule ambao sadaka za Wayahudi zilifanyiwa, ni nani angekubaliwa? **{SLsw 29.1}**

Kwa uangalifu mkubwa Wakristo wanapaswa kudhibiti mazoea yao, ili waweze kuhifadhi nguvu kamili za kila uwezo kwa ajili ya huduma ya Kristo. Ikiwa

tunataka kutakaswa katika nafsi, mwili, na roho, ni lazima tuishi kwa kupatana na sheria ya Mungu. Moyo hauwezi kudumisha hali ya kujiweka wakfu kwa Mungu huku tamaa za chakula na za mwili zikijiridhishwa kwa gharama ya afya na maisha. Wale wanaokiuka sheria ambazo afya inategemea ni lazima wateseke kwa sababu hiyo. Wamepunguza uwezo wao kwa kila namna, kiasi kwamba hawawezi kutimiza ipasavyo wajibu wao kwa wanadamu wenzao, na hivyo hushindwa kabisa kuitikia madai ya Mungu. **{SLsw 29.2}**

Lord Palmerston, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, alipoombwa na makasisi wa Scotland ateue siku ya kufunga na kuomba ili kuzuia kipindupindu, alijibu kwa maana hii: ***"Safisheni na kuua vijidudu katika barabara na nyumba zenu, himizeni usafi na afya miongoni mwa maskini, na hakikisheni kwamba wanapatiwa chakula bora na mavazi ya kutosha, na kwa ujumla tumieni hatua zinazofaa za usafi wa mazingira; ndipo hamtakuwa na sababu ya kufunga na kuomba. Wala Bwana hatawasikia maombi yenu wakati hatua hizi za kinga alizoweka zinapuuzwa."*** **{SLsw 30.1}**

Paulo anasema, ***"Na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukikamilisha/tukitimiza***

utakatifu katika kumcha Mungu.” (2 Wakorintho 7:1). Anaweka mbele yetu, kwa kututia moyo, uhuru unaofurahiwa na wale waliotakaswa kweli: ***“Basi, sasa hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho”*** (Warumi 8:1). Anawaagiza Wagalatia, ***“Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili”*** (Wagalatia 5:16). Mtume anataja baadhi ya namna za tamaa za mwili—***“ibada ya sanamu, ...ulevi, ...na mambo yanayofanana na hayo”*** (mistari ya 20, 21). Na baada ya kutaja matunda ya Roho, ambalo miongoni mwa hayo ni kiasi, anaongeza, ***“Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake”*** (mstari wa 24). **{SLsw 30.2}**

Tumbaku

Yakobo anasema kwamba hekima itokayo juu ni ***“kwanza ni safi”*** (Yakobo 3:17). Ikiwa angewaona ndugu zake wakitumia tumbaku, je, hangekemea mazoea hayo kuwa ni ***“ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, ya Shetani”*** (mstari wa 15)? Katika zama hizi za nuru ya Kikristo, ni mara ngapi midomo inayolitaja Jina la thamani la Kristo huchafuliwa na mate yanayotemwa wakati wa kutafuna

tumbaku/ugoro, na pumzi huchafuliwa na uvundo wake! Hakika, nafsi inayoweza kufurahia uchafu wa namna hiyo lazima nayo iwe imenajisika. Nimewaona watu waliodai kufurahia baraka ya utakaso kamili, huku wakiwa watumwa wa tumbaku na kuleta uchafuzi kwa kila kitu kilichowazunguka; nami nimejiuliza, Mbingu ingekuwaje ikiwa kungekuwa humo watumiaji wa tumbaku? Neno la Mungu limetangaza wazi kwamba ***"hakitaingia humo kamwe chochote kitiacho unajisi"*** (Ufunuo 21:27). Itakuwaje basi, kwa wale wanaojiingiza katika mazoea haya machafu wanawezaje kutumaini kukubaliwa humo? **{SLsw 30.3}**

Watu wanaodai kumcha Mungu huitoa miili yao juu ya madhabahu ya Shetani na kuchoma uvumba wa tumbaku kwa ajili ya "ukuu wake wa kishetani." Je, kauli hii inaonekana kuwa kali? Bila shaka, sadaka hiyo hutolewa kwa mungu fulani. Kwa kuwa Mungu ni safi na mtakatifu, naye hatakubali chochote kilicho na uchafu katika tabia yake, ni lazima aikatae sadaka hii ya gharama kubwa, chafu, na isiyo takatifu; kwa hiyo tunahitimisha kwamba Shetani ndiye anayedai heshima hiyo. **{SLsw 31.1}**

Yesu alikufa ili kumwokoa mwanadamu kutoka katika mshiko wa Shetani. Alikuja kutuweka huru kwa damu ya dhabihu Yake ya upatanisho. Mtu ambaye amekuwa mali ya Yesu Kristo, na ambaye mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu, hatakuwa mtumwa wa mazoea yenye madhara yenye kufisha/kusumisha ya kutumia tumbaku. Nguvu zake ni za Kristo, aliyemnunua kwa gharama ya damu. Mali yake ni ya Bwana. Basi, anawezaje kuwa hana hatia kwa kutumia kila siku rasilimali alizokabidhiwa na Bwana ili kutosheleza hamu ambayo haina msingi wa kimaumbile? **{SLsw 31.2}**

Kiasi kikubwa sana cha fedha hupotezwa kila mwaka kwa ajili ya kujiridhisha huku, huku roho zikiangamia kwa kukosa Neno la uzima. Wakristo wanaodai kumcha Mungu humwibia Mungu katika zaka na sadaka, huku kwenye madhabahu ya tamaa yenye kuangamiza, kwa kutumia tumbaku, wakiweka fedha nyingi zaidi kuliko wanazotoa kuwasaidia maskini au kukidhi mahitaji ya kazi ya Mungu. Wale waliotakaswa Kweli watashinda kila tamaa yenye madhara. Ndipo mikondo ya fedha hizi zilizokuwa zikitumiwa katika matumizi yasiyo ya lazima zitaelekezwa katika hazina ya Bwana, na Wakristo watakuwa mstari wa mbele katika kujikana nafsi, kujitoa

mhanga, na kuwa na kiasi. Ndipo watakuwa nuru ya ulimwengu. **{SLsw 32.1}**

Chai na Kahawa

Chai na kahawa, pamoja na tumbaku, vina madhara kwa mwili. Chai hulevya. Ingawa athari yake si kali kwa kiwango kilekile, kwa namna ya athari yake inafanana na ile ya vileo/pombe. Kahawa ina mwelekeo mkubwa zaidi wa kufifisha akili na kudhoofisha nguvu. Haina nguvu nyingi kama tumbaku, lakini athari yake inafanana nayo. Hoja zinazotolewa dhidi ya matumizi ya tumbaku zinaweza pia kutolewa dhidi ya matumizi ya chai na kahawa. **{SLsw 32.2}**

Wale waliozoea kutumia chai, kahawa, tumbaku, kasumba/banghi, au vileo wanaponyimwa kile walichozoea kujiridhisha nacho, huona kuwa haiwezekani kushiriki kwa shauku na bidii katika ibada ya Mungu. Neema ya Mungu huonekana kutokuwa na uwezo wa kuyahuisha au kuyafanya maombi yao na ushuhuda wao kuwa wa kiroho. Wakristo hawa wanaodai kuwa wacha Mungu wanapaswa kujiuliza: Chanzo cha furaha yao ni nini? Je, kinatoka juu au chini? **{SLsw 32.3}**

Kwa mtumiaji wa vichocheo, kila kitu huonekana kuwa hakina ladha bila kujiridhisha kwa kitu

anachokipenda sana. Hali hii hufifisha hisia za asili za mwili na akili, na humfanya asiwe tayari kupokea ushawishi wa Roho Mtakatifu. Anapokosa kichocheo alichozoea, mwili na nafsi yake huwa na njaa, na siyo njaa ya haki, si ya utakatifu, wala si ya uwepo wa Mungu, bali ya sanamu yake anayoithamini. Kwa kujiridhisha katika tamaa zenye madhara, Wakristo wanaodai kuwa wacha Mungu hudhoofisha nguvu zao kila siku, na hivyo kuwafanya wasiweze kumtukuza Mungu. **{SLsw 32.4}**

SURA YA 4—TANURU LA MOTO

Katika mwaka uleule ambao Danieli na wenzake waliingia katika utumishi wa mfalme wa Babeli, matukio yalitokea ambayo yaliujaribu sana uadilifu wa vijana hawa Waebrania na kuthibitisha mbele ya taifa lililoabudu sanamu nguvu na uaminifu wa Mungu wa Israeli. **{SLsw 34.1}**

Mfalme Nebukadneza alipokuwa akiutazamia wakati ujao kwa wasiwasi mkubwa, alipata ndoto ya ajabu

iliyomsumbua sana, ***"na usingizi wake ukamwacha"*** (Danieli 2:1). Ingawa maono hayo ya usiku yalikuwa na athari kubwa akilini mwake, alishindwa kukumbuka mambo yote yaliyohusu ndoto hiyo. Aliwaita wanajimu na wachawi wake, na kwa kuwaahidi utajiri na heshima nyingi, akawaamuru wamwambie ndoto yake pamoja na tafsiri yake. Lakini wao wakasema, ***"tuambie sisi watumishi wako ile ndoto, nasi tutakuonyesha tafsiri yake."*** (mstari wa 4). **{SLsw 34.2}**

Mfalme alijua kwamba ikiwa wangeweza kweli kueleza tafsiri ya ndoto hiyo, wangeweza pia kusema ndoto yenyewe. Kwa majaliwa Yake, Bwana alikuwa amempa Nebukadneza ndoto hiyo na akaruhusu maelezo yake yasahaulike, huku akiacha moyoni mwake hisia yenye kutisha, ili kufichua madai ya watu wenye hekima wa Babeli. Mfalme alikasirika sana na kutishia kwamba wote wangeuawa ikiwa, ndani ya muda uliowekwa, ndoto hiyo isingeweza kufunuliwa. Danieli na wenzake walipaswa kuuawa pamoja na manabii hao wa uongo; lakini Danieli, akihatarisha maisha yake, alithubutu kuingia mbele ya mfalme na kuomba apewe muda ili aweze kumwonyesha ndoto hiyo pamoja na tafsiri yake. **{SLsw 34.3}**

Mfalme akakubali ombi hilo. Ndipo Danieli akawakusanya wenzake watatu, nao kwa pamoja wakalipeleka jambo hilo mbele za Mungu, wakitafuta hekima kutoka kwa Chanzo cha nuru na maarifa. Ingawa walikuwa katika ikulu ya mfalme, wakiwa wamezungukwa na vishawishi, hawakusahau wajibu wao kwa Mungu. Walipata nguvu kutokana na ufahamu kwamba majaliwa ya Mungu yalikuwa yamewaweka mahali walipokuwa; kwamba walikuwa wakifanya kazi Yake na kutenda kulingana na madai ya Kweli na wajibu. Walikuwa na imani thabiti kwa Mungu. Walipokuwa katika hali ya mashaka na hatari, walimgeukia Yeye ili awape nguvu, naye alikuwa msaada wao wa daima na wa karibu. **{SLsw 35.1}**

Siri Yafunuliwa

Watumishi wa Mungu hawakumwomba bure. Walikuwa wamemtukuza, naye katika saa ya majaribu akawatukuza. Siri ilifunuliwa kwa Danieli, naye akaharakisha kuomba kukutana na mfalme. **{SLsw 35.2}**

Mateka huyo Myahudi anasimama mbele ya mfalme wa milki yenye nguvu zaidi ambayo jua limewahi kuiangaza. Mfalme yuko katika dhiki kubwa katikati ya

utajiri na utukufu wake wote, lakini yule kijana aliyehamishwa yuko katika amani na furaha katika Mungu wake. Sasa, ikiwa kuna wakati wa Danieli kujitukuza, huo ulikuwa ndio wakati. Angeweza kuonyesha wema wake mwenyewe na hekima yake iliyo bora. Lakini kwanza kabisa anakataa kujitwalia heshima yoyote na kumtukuza Mungu kuwa Chanzo cha hekima: **{SLsw 35.3}**

"Ile siri aliyoiuliza mfalme, wenye hekima hawawezi kumfunulia mfalme; wala wachawi, wala waganga, wala wanajimu; lakini Yuko Mungu mbinguni afunuaye siri, naye amemjulisha mfalme Nebukadreza mambo yatakayokuwa siku za mwisho." (Danieli 2:27, 28). Mfalme anasikiliza kwa makini sana na kwa kicho, huku kila maelezo ya ndoto yakielezwa upya mbele yake; na tafsiri hiyo inapotolewa kwa uaminifu, anaona kwamba anaweza kuitegemea kuwa ni ufunuo wa Mungu. **{SLsw 36.1}**

Kweli kuu zenye uzito zilizowasilishwa katika maono hayo ya usiku zinaacha athari kubwa katika akili ya mfalme. Kwa unyenyekevu na kicho, anaanguka chini na kuabudu, akisema: ***"Hakika Mungu wenu Ndiye***

Mungu wa miungu, na Bwana wa wafalme, awezaye kufumbua siri." (mstari wa 47). **{SLsw 36.2}**

Sanamu ya Dhahabu

Nuru iliyotoka moja kwa moja kutoka Mbinguni iliruhusiwa kumwangazia Mfalme Nebukadneza, na kwa muda mfupi aliathiriwa na kicho/hofu ya Mungu. Lakini miaka michache ya mafanikio ilijaza moyo wake kiburi, naye akasahau kumkiri Mungu aliye hai. Akaanza tena ibada yake ya sanamu kwa bidii kubwa na ushupavu wa kidini wa kupita kiasi. **{SLsw 36.3}**

Kutokana na hazina alizopata vitani, alitengeneza sanamu ya dhahabu iliyowakilisha ile sanamu aliyokuwa ameiona katika ndoto yake, akaiweka katika uwanda wa Dura, na kuwaamuru watawala wote pamoja na watu wote waiabudu, la sivyo wangeuawa. Sanamu hiyo ilikuwa na urefu wa karibu futi tisini na upana wa futi tisa, na kwa mtazamo wa taifa hilo lililoabudu sanamu, ilikuwa na mwonekano wa kuvutia na wa kifahari sana. Tangazo likatolewa likiwataka maafisa wote wa ufalme wakusanyike wakati wa kuwekwa wakfu kwa sanamu hiyo, na mara tu vyombo vya muziki viliposikika, wainame na kuiabudu. Mtu yeyote ambaye angekataa

kufanya hivyo alipaswa kutupwa mara moja katikati ya tanuru ya moto iliyokuwa ikiwaka. **{SLsw 36.4}**

Siku iliyowekwa ilifika, na umati mkubwa ulikuwa umekusanyika. Ndipo mfalme akaarifiwa kwamba wale Waebrania watatu aliokuwa amewaweka juu ya jimbo la Babeli walikuwa wamekataa kuiabudu sanamu hiyo. Hawa walikuwa wenzake watatu wa Danieli, ambao mfalme alikuwa amewapa majina ya Shadraka, Meshaki, na Abednego. Akiwa amejawa na hasira, mfalme wa himaya akawaita mbele yake na, akielekeza kwenye tanuru iliyokuwa ikiwaka kwa ukali, akawaambia juu ya adhabu ambayo wangepata ikiwa wangekataa kutii amri yake. **{SLsw 37.1}**

Vitisho vya mfalme vilikuwa bure. Hakuweza kuwageuza watu hao bora, mashuhuri na waungwana kutoka katika uaminifu wao kwa Mtawala mkuu wa mataifa. Kutokana na historia ya baba zao, walikuwa wamejifunza kwamba kutomtii Mungu ni aibu, maafa na uharibifu; na kwamba kumcha Bwana si mwanzo wa hekima tu, bali pia ni msingi wa ustawi wote wa kweli. Walitazama kwa utulivu tanuru ya moto na umati wa waabudu sanamu. Walikuwa wamemtumaini Mungu, na walikuwa na hakika kwamba hatawaacha sasa. Jibu lao

lilikuwa la heshima, lakini lenye msimamo thabiti: ***"Ujue, Ee mfalme, ya kuwa sisi hatukubali kuitumikia miungu yako, wala kuisujudia hiyo sanamu ya dhahabu uliyoisimamisha."*** (Danieli 3:18). **{SLsw 37.2}**

Mfalme huyo mwenye kiburi alikuwa amezungukwa na watu wake wakuu, maafisa wa serikali, na jeshi lililokuwa limeyashinda mataifa; nao wote waliungana kumsifu kana kwamba alikuwa na hekima na nguvu za miungu. Katikati ya onyesho hilo lenye kuvutia na lenye msukumo, wale vijana watatu Waebrania walisimama, wakiendelea kwa uthabiti kukataa kutii amri ya mfalme. Walikuwa wametii sheria za Babeli kadiri sheria hizo hazikupingana na madai ya Mungu; lakini hawakuwa tayari kuyumbishwa hata sentimeta moja, kutoka katika wajibu waliokuwa nao kwa Muumba wao. **{SLsw 37.3}**

Hasira ya mfalme haikuwa na mipaka. Katika kilele cha nguvu na utukufu wake, kukaidiwa hivyo na wawakilishi wa taifa lililodharauliwa na lililokuwa utumwani kulikuwa tusi ambalo moyo wake wenye kiburi usingeweza kulivumilia. Tanuru ilikuwa imechochewa moto mara saba zaidi ya kawaida, nao mateka hao Waebrania wakatupwa ndani yake. Miali ya moto ilikuwa

mikali sana kiasi kwamba wale watu waliowatupa ndani wakaungua na kufa. **{SLsw 38.1}**

Mbele za Yule Asiye na Kikomo

Ghafla uso wa mfalme ukapauka kwa hofu. Macho yake yakakazia miali iliyokuwa ikiwaka, kisha akawageukia wakuu wake na kusema, **"Je! Hatukutupa watu watatu, hali wamefungwa, katikati ya moto?"** (mstari wa 24). Wakajibu, **"Kweli, Ee mfalme."** Ndipo mfalme akasema, ***"Tazama, mimi naona watu wanne, nao wamefunguliwa, wanatembea katikati ya moto hali hawana dhara; na sura yake Yule wa nne ni mfano wa Mwana wa miungu."*** (mstari wa 25). **{SLsw 38.2}**

Kristo anapojidhihirisha kwa wana wa wanadamu, nguvu isiyoonekana hunena na nafsi zao. Wanajihisi kuwa wako katika uwepo wa Yule asiye na kikomo. Mbele ya ukuu Wake, wafalme na wakuu hutetemeka na kukiri kwamba Mungu aliye hai Yuko juu ya kila mamlaka ya kidunia. **{SLsw 38.2}**

Akiwa amejawa na majuto na aibu, mfalme akasema, ***"Enyi watumishi wa Mungu Aliye juu, tokeni, mje huku"*** (mstari wa 26). Nao wakatoka na kujionyesha mbele ya umati huo mkubwa bila kudhurika; hata harufu ya moto haikuwa imeambatana na mavazi yao. Muujiza

huu ulileta mabadiliko makubwa katika fikra za watu. Sanamu ile kubwa ya dhahabu, iliyokuwa imewekwa kwa maonyesho makubwa ya fahari, ilisahaulika. Mfalme akatoa amri kwamba mtu yeyote atakayenena kinyume cha Mungu wa watu hawa auawe, ***"kwa kuwa hakuna Mungu mwingine awezaye kuokoa namna hii"*** (mstari wa 29). **{SLsw 39.1}**

Uadilifu Imara na Maisha Yaliyotakaswa

Waebrania hawa watatu walikuwa na utakaso wa kweli. Kanuni ya Kweli ya Kikristo haisiti wala kujishughulisha na kupima matokeo au adhabu. Haiulizi, *"Watu watafikiri nini kunihusu nikifanya hivi?"* au, *"Hili litaathirije hali yangu ya kidunia nikifanya lile?"* Kwa shauku kubwa sana, watoto wa Mungu hutamani kujua kile ambacho Mungu angependa wafanye, ili matendo yao yamtukuze. Bwana ametoa kila kitu kinachohitajika ili mioyo na maisha ya wafuasi Wake wote yaweze kutawaliwa na neema ya Mungu, ili wawe kama taa zinazowaka na kung'aa ulimwenguni. **{SLsw 39.2}**

Waebrania hawa waaminifu walikuwa na uwezo mkubwa wa asili, walikuwa wamepata mafunzo ya juu kabisa ya kiakili, na sasa walikuwa wameshika nafasi ya heshima; lakini mambo hayo yote hayakuwaongoza

kumsahau Mungu. Uwezo wao uliwekwa chini ya nguvu ya neema ya Mungu inayotakasa. Kupitia uadilifu wao thabiti, walidhihirisha sifa za Yule aliyewaita kutoka gizani na kuwaingiza katika nuru Yake ya ajabu. Katika ukombozi wao wa ajabu, nguvu na ukuu wa Mungu vilidhihirishwa mbele ya kusanyiko lile kubwa. Yesu alisimama kando yao katika tanuru ya moto, na kwa utukufu wa uwepo Wake, /akamthibithishia mfalme mwenye kiburi wa Babeli kwamba huyo hakuwa mwingine ila **Mwana wa Mungu**. Nuru ya Mbinguni ilikuwa iking'aa kutoka kwa Danieli na wenzake, mpaka wote waliokuwa pamoja nao wakaielewa imani iliyoyatukuza maisha yao na kupamba tabia zao. Kwa kuwaokoa watumishi Wake waaminifu, Bwana anatangaza kwamba atasimama pamoja na wanaodhulumiwa na kuyapindua mamlaka yote ya kidunia yanayokanyaga mamlaka ya Mungu wa Mbinguni. **{SLsw 39.3}**

Somo kwa Wenye Moyo wa Kukata Tamaa

Ni somo kubwa lililoje tunalopata hapa kwa ajili ya wenye mioyo dhaifu, yenye kukata tamaa kirahisi, na yenye kusitasita, na watu walio waoga katika kazi ya Mungu! Ni faraja iliyoje kwa wale ambao hawaruhusu

vitisho wala hatari viwageuze kutoka katika wajibu wao! Wahusika hawa waaminifu na thabiti ni mifano ya utakaso, ingawa hawakuwa na wazo la kudai heshima hiyo kubwa. Kiasi cha mema kinachoweza kutendwa na Wakristo wanaoonekana kuwa watu wa kawaida au wasiojulikana na watu, lakini waliojitolea kwa Mungu hakiwezi kukadiriwa mpaka kumbukumbu za maisha yao zitakapofunuliwa, wakati hukumu itakapoketi na vitabu vitakapofunguliwa. **{SLsw 40.1}**

Kristo anajihusianisha na watu wa namna hii; haoni haya kuwaita ndugu. Ambapo sasa miongoni mwetu yuko mmoja, wangepaswa kuwepo mamia walio karibu sana na Mungu, ambao maisha yao yangekuwa katika upatanifu kamili na mapenzi Yake, hivi kwamba wangekuwa taa zinazowaka na kuangaza, wakiwa wametakaswa kabisa katika nafsi, mwili, na roho. **{SLsw 40.2}**

Vita bado vinaendelea kati ya watoto wa nuru na watoto wa giza. Wale wanaolitaja Jina la Kristo wanapaswa kujiondolea ulegevu unaodhoofisha juhudi zao, na kukabiliana na majukumu mazito yaliyowekwa juu yao. Wote watakaofanya hivyo wanaweza kutarajia nguvu za Mungu kudhihirishwa ndani yao. Mwana wa Mungu, Mkombozi wa ulimwengu, atawakilishwa katika

maneno na matendo yao, na Jina la Mungu litatukuzwa. **{SLsw 41.1}**

Kama ilivyokuwa katika siku za Shadraka, Meshaki, na Abednego, ndivyo itakavyokuwa katika kipindi cha mwisho cha historia ya dunia: Bwana atatenda kwa nguvu kwa ajili ya wale wanaosimama imara upande wa yaliyo sahihi. Yeye aliyetembea pamoja na mashujaa hao Waebrania katika tanuru ya moto atakuwa pamoja na wafuasi Wake popote watakapokuwa. Uwepo Wake wa kudumu utawafariji na kuwategemeza. Katikati ya wakati wa taabu—taabu ambayo haijawahi kutokea tangu kuwapo kwa taifa—wateule Wake watasimama bila kutikisika. Shetani pamoja na majeshi yote ya uovu hawezi kumwangamiza hata yule aliye dhaifu zaidi miongoni mwa watakatifu wa Mungu. Malaika walio na nguvu kuu watawalinda, na kwa ajili yao Yehova atajidhihirisha kuwa **"Mungu wa miungu,"** Mwenye uwezo wa kuwaokoa kabisa wale waliomtumaini. —*Prophets and Kings*, uk. 513. **{SLsw 41.2}**

SURA YA 5—DANIELI KATIKA TUNDU LA SIMBA

Dario alipochukua utawala wa Babeli, mara moja alianza kuupanga upya utawala huo. Aliweka ***"maliwali mia na ishirini, wawe juu ya ufalme wote; na juu yao akaweka wakubwa watatu, na Danieli alikuwa mmoja wao."*** (Danieli 6:1, 2). Na ***"Danieli huyo alipata sifa kuliko wakubwa na maliwali, kwa kuwa roho bora ilikuwa ndani yake; naye mfalme akaazimu kumweka juu ya ufalme wote."*** (mstari wa 3). Heshima alizopewa Danieli ziliamsha wivu wa viongozi wakuu wa ufalme. Wakuu na maliwali wakatafuta sababu ya kumshitaki.

"lakini hawakuweza kuona sababu wala kosa; kwa maana alikuwa mwaminifu, wala halikuonekana kosa wala hatia ndani yake." (mstari wa 4). **{SLsw 42.1}**

Ni somo kubwa lililoje tunalopatiwa hapa kwa ajili ya Wakristo wote! Macho makali ya wivu yalikuwa yamemkazia Danieli siku baada ya siku; uchunguzi wao ulizidi kuwa mkali kwa sababu ya chuki, lakini hawakuweza kuonyesha kwamba lipo neno wala tendo lolote katika maisha yake lilikuwa baya. Hata hivyo, Danieli hakudai kuwa ametakaswa; bali alifanya jambo lililokuwa bora zaidi kwa kiwango kisichopimika—aliishi maisha ya uaminifu na kujiweka wakfu kwa Mungu. **{SLsw 42.}**

Kadiri mwenendo wa Danieli ulivyokuwa usio na lawama, ndivyo chuki ambayo maadui zake walikuwa nayo dhidi yake ilivyozidi kuwa kubwa. Walijawa na ghadhabu na wendawazimu kwa sababu hawakuweza kupata jambo lolote katika tabia yake ya kimaadili au katika kutekeleza wajibu wake ambalo wangeweza kulitumia kama msingi wa kumshitaki. ***"Ndipo wale watu wakasema, Hatutapata sababu ya kumshitaki Danieli huyo, tusipoipata/isipokuwa katika mambo ya sheria ya Mungu wake."*** (mstari wa 5). Danieli alisali kwa Mungu

wa mbinguni mara tatu kwa siku. Hilo ndilo lililokuwa shtaka pekee ambalo wangeweza kulileta dhidi yake. **{SLsw 43.1}**

Ndipo wakapanga hila ya kumwangamiza. Maadui zake wakakusanyika katika ikulu na kumsihi mfalme atoe amri kwamba hakuna mtu katika ufalme wote ambaye angeomba jambo lolote kwa Mungu au kwa mwanadamu yeyote, isipokuwa kwa Mfalme Dario, kwa muda wa siku thelathini; na kwamba yeyote ambaye angekiuka amri hiyo atupwe katika tundu la simba. Mfalme hakujua chochote kuhusu chuki ya watu hao dhidi ya Danieli, wala hakushuku kwamba amri hiyo ingemdhuru kwa namna yoyote. Kwa kutumia maneno ya /kujikomba, walimfanya mfalme aamini kwamba kutoa amri hiyo kungekuwa jambo la kumletea heshima kubwa. Wakiwa na tabasamu la ushindi wa kishetani nyusoni mwao, walitoka mbele ya mfalme na kufurahi pamoja juu ya mtego waliokuwa wamemtayarishia mtumishi wa Mungu. **{SLsw 43.2}**

Mfano wa Ujasiri na Uaminifu

Amri inatolewa na mfalme. Danieli anafahamu kusudi la maadui zake la kumwangamiza. Lakini habadili mwenendo wake hata katika jambo moja. Kwa utulivu anatekeleza majukumu yake ya kawaida, na wakati wa

sala huenda katika chumba chake. Akiwa amefungua madirisha yake kuelekea Yerusalemu, anamtolea Mungu wa mbinguni maombi yake. Kwa mwenendo wake huo, anatangaza bila woga kwamba hakuna mamlaka ya kidunia iliyo na haki ya kujiingiza kati yake na Mungu wake na kumwambia ni nani anayepaswa kumwomba na ni nani asiyepaswa kumwomba. Jamani! mtu huyo alikuwa mwenye msimamo thabiti! Leo anasimama mbele ya ulimwengu kama mfano unaostahili kupongezwa wa ujasiri na uaminifu wa Kikristo. Anamgeukia Mungu kwa moyo wake wote, ingawa anajua kwamba kujitoa kwake kwa Mungu kunaweza kumgharimu maisha yake. **{SLsw 43.3}**

Maadui zake wanamchunguza siku nzima. Mara tatu huenda katika chumba chake, na mara tatu sauti ya maombi ya dhati inasikika. Asubuhi iliyofuata, shtaka linapelekwa kwa mfalme kwamba Danieli, mmoja wa mateka wa Yuda, amekaidi amri yake. Mfalme aliposikia maneno hayo, mara moja akatambua mtego waliokuwa wamemtegea. Alijuta sana kwa kuwa alikuwa ametoa amri hiyo, naye akahangaika mpaka jua lilipozama, akitafuta mpango ambao ungemwezesha Danieli kuokolewa kutoka kwenye huu mtego. Lakini maadui wa nabii walikuwa wametangulia kulitarajia jambo hilo, nao

wakaja mbele ya mfalme na kusema: **“Ee mfalme, ujue ya kuwa ni sheria ya Wamedi na Waajemi, lisibadilike neno lo lote lililo marufuku, wala amri yo yote iliyowekwa na mfalme.”** **{SLsw 44.1}**

Ndipo mfalme akaamuru, nao wakamleta Danieli na kumtupa katika tundu la simba. Kisha mfalme akamwambia Danieli, ***“Mungu wako, ambaye unamtumikia daimgfa, Yeye atakuponya”*** (mistari ya 15, 16). Jiwe likawekwa juu ya mdomo wa lile tundu, na kutiwa muhuri kwa pete ya kifalme. ***“Kisha mfalme akaenda nyumbani kwake, akakesha usiku kucha, akafunga; na vinanda havikuletwa mbele yake; na usingizi wake ukampaa.”*** (mstari wa 18). **{SL 44.2}**

“Mungu Wangu Amemtuma Malaika Wake”

Mapema asubuhi, mfalme aliharakisha kwenda kwenye tundu la simba, akaita kwa sauti, ***“Danieli, Ee Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, je! Mungu wako, unayemtumikia daima, aweza kukuponya na simba hawa?”*** (mstari wa 20). Sauti ya nabii ikasikika ikijibu, ***“Ee mfalme, uishi milele. Mungu wangu amemtuma malaika Wake, Naye ameyafumba makanwa ya simba, nao hawakunidhuru; kwa kuwa mbele zake mimi***

nalionekana kuwa sina hatia; tena, mbele yako, Ee mfalme, sikukosa neno." **{SLsw 45.1}**

"Basi mfalme akafurahi sana, akaamuru wamtoe Danieli katika lile tundu. Ndipo Danieli akatolewa katika lile tundu, wala dhara lo lote halikuonekana mwilini mwake, kwa sababu alikuwa anamtumaini Mungu wake." (mistari ya 22, 23). Hivyo, mtumishi wa Mungu akaokolewa. Na mtego ambao maadui zake walikuwa wamemtegea ili wamwangamize ukawa sababu ya maangamizi yao wenyewe. Kwa amri ya mfalme, wakatupwa katika lile tundu, na mara moja wakaliwa na wanyama hao wakali. **{SLsw 45.2}**

SURA YA 6—MAOMBI YA DANIELI

Kadiri mwisho wa miaka sabini ya utumwa ulivyokuwa ukikaribia, Danieli alishughulika sana katika kutafakari unabii wa Yeremia. Aliona kwamba wakati ulikuwa umekaribia ambapo Mungu angewapa watu Wake waliochaguliwa kipindi kingine cha majaribu; naye kwa kufunga, kujinyenyekeza, na kusali, alimsihi Mungu wa mbinguni kwa ajili ya Israeli, akisema: ***"Ee Bwana, Mungu mkuu, Mwenye kutisha, Ashikaye maagano na rehema kwao wampendao, na kuzishika amri Zake; tumefanya dhambi, tumefanya ukaidi, tumetenda maovu, tumeasi, naam, hata kwa kuyaacha maagizo Yako na hukumu Zako; wala hatukuwasikiliza watumishi Wako, manabii, ambao kwa Jina Lako walisema na wafalme wetu, na wakuu wetu, na baba zetu, na watu wote wa nchi."*** (Danieli 9:4–6). **{SLsw 46.1}**

Danieli hajitangazi mbele za Bwana kuwa yeye ni mwaminifu. Badala ya kudai kuwa yeye ni safi na

mtakatifu, nabii huyu mwenye kuheshimiwa anajihesabu kwa unyenyekevu kuwa miongoni mwa wenye dhambi wa Israeli. Hekima ambayo Mungu alikuwa amempa ilikuwa ya juu sana kuliko hekima ya watu wakuu wa ulimwengu, kama vile nuru ya jua linalong'aa angani wakati wa adhuhuri ilivyo angavu zaidi kuliko nuru ya nyota iliyo hafifu kabisa. Hata hivyo, tafakari sala iliyotoka katika midomo ya mtu huyu aliyependelewa sana na Mbinguni. Kwa unyenyekevu mkuu, kwa machozi na kwa moyo uliopondeka, anamsihi Mungu kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya watu wake. Anaifungua nafsi yake mbele za Mungu, akikiri kutostahili kwake na kutambua ukuu na enzi ya Bwana. **{SLsw 46.2}**

Bidii na Ari

Ni bidii na ari kubwa kiasi gani vinavyoonekana katika maombi yake! Mkono wa imani unanyoshwa juu ili kushikilia ahadi zisizoshindwa kamwe za Yeye Aliye Juu! Nafsi yake inahangaika kwa uchungu mkuu. Naye ana ushahidi kwamba sala yake imesikiwa. Anajua kwamba ushindi ni wake. Ikiwa sisi kama watu tungeomba kama Danieli alivyoomba, na kupambana kama alivyopambana, huku tukizinyenyekeza nafsi zetu mbele za Mungu,

tungeona majibu dhahiri ya maombi yetu, kama yale aliyopewa Danieli. Sikiliza jinsi anavyowasilisha ombi lake mbele ya mahakama ya mbinguni: **{SLsw 47.1}**

"Ee Bwana, Mungu mkuu, mwenye kutisha, ashikaye maagano na rehema kwao wampendao, na kuzishika amri zake; tumefanya dhambi, tumefanya ukaidi, tumetenda maovu, tumeasi, naam, hata kwa kuyaacha maagizo yako na hukumu zako; wala hatukuwasikiliza watumishi Wako, manabii, ambao kwa Jina Lako walisema na wafalme wetu, na wakuu wetu, na baba zetu, na watu wote wa nchi." (mistari ya 18, 19). **{SLsw 47.2}**

Mtu wa Mungu alikuwa akiomba baraka ya Mbinguni juu ya watu wake na ujuzi ulio wazi zaidi wa mapenzi ya Mungu. Mzigo wa moyo wake ulikuwa kwa ajili ya Israeli, ambao, kwa maana kamili kabisa, hawakuwa wakishika sheria ya Mungu. Anakiri kwamba misiba yao yote iliwapata kwa sababu ya kuikiuka sheria hiyo takatifu. Anasema, ***"Tumetenda maovu. Ee Bwana sawasawa na haki yako yote, nakusihi, hasira yako na ghadhabu yako zigeuzwe na kuuacha mji wako Yerusalemu, mlima wako mtakatifu; maana kwa sababu ya dhambi zetu, na maovu ya baba zetu, Yerusalemu na***

watu wako wamepata kulaumiwa na watu wote wanaotuzunguka." (mistari ya 15, 16). Wayahudi walikuwa wamepoteza tabia yao ya pekee na takatifu kama watu waliochaguliwa na Mungu. ***"Basi sasa, Ee Mungu wetu, yasikilize maombi ya mtumishi Wako, na dua zake, ukaangazishe uso Wako juu ya Patakatifu pako palipo ukiwa."*** (mstari wa 17). Moyo wa Danieli ulijawa na shauku kubwa kwa ajili ya Patakatifu pa Mungu palipokuwa ukiwa. Alijua kwamba ustawi wa Patakatifu hapo ungeweza kurejeshwa tu ikiwa Israeli wangetubu kwa sababu ya kuzivunja sheria za Mungu, na kuwa wanyenyekevu, waaminifu, na watiifu. **{SLsw 47.3}**

Mjumbe wa Mbinguni

Danieli alipokuwa akiendelea kusali, malaika Gabrieli alishuka upesi kutoka katika makao ya mbinguni ili kumwambia kwamba maombi yake yamesikiwa na kujibiwa. Malaika huyu mwenye nguvu alikuwa ametumwa kumpa Danieli ustadi na ufahamu—kumfunulia mafumbo ya nyakati zijazo. Hivyo, wakati Danieli alipokuwa akitafuta kwa bidii kujua na kuelewa ukweli, aliletwa katika mawasiliano na mjumbe wa Mbinguni aliyeteuliwa. **{SLsw 48.1}**

Kwa kujibu ombi lake, Danieli alipokea si nuru na ukweli tu ambao yeye na watu wake walikuwa wakiuhitaji sana, bali pia alionyeshwa matukio makuu ya wakati ujao, hata kufikia wakati wa ujio wa Mkombozi wa ulimwengu. Wale wanaodai kuwa wametakaswa, ilhali hawana shauku ya kuyachunguza Maandiko wala kung'ang'ana na Mungu katika sala ili kupata uelewa ulio wazi zaidi wa ukweli wa Biblia, hawajui utakaso wa kweli ni nini. **{SLsw 48.2}**

Danieli alizungumza na Mungu. Mbingu ilifunguka mbele yake. Lakini heshima kuu alizopewa zilitokana na unyenyekevu wake na kumtafuta Mungu kwa bidii. Wote wanaoliamini Neno la Mungu kwa moyo watakuwa na njaa na kiu ya kujua mapenzi Yake. Mungu Ndiye Chanzo cha ukweli. Huiangazia akili iliyotiwa giza na kuipa akili ya mwanadamu uwezo wa kuushika na kuuelewa Ukweli ambao Yeye ameufunua. **{SLsw 49.1}**

Kumtafuta Mungu kwa Hekima

Katika tukio lililoelezwa hivi punde, malaika Gabrieli alimpa Danieli maelekezo yote ambayo kwa wakati huo angekuwa na uwezo wa kuyapokea. Hata hivyo, miaka michache baadaye, nabii huyo alitamani kujifunza zaidi kuhusu mambo ambayo yalikuwa bado hayajaelezwa

kikamilifu, naye tena akaazimia kumtafuta Mungu ili kupata nuru na hekima. ***"Katika siku zile mimi, Danieli, nalikuwa nikiomboleza muda wa majuma matatu kamili. Sikula chakula kitamu, wala nyama wala divai haikuingia kinywani mwangu, wala sikujipaka mafuta kabisa, hata majuma matatu kamili yalipotimia. Na siku ya ishirini na nne ya mwezi wa kwanza, nilipokuwa kando ya ule mto mkubwa, Hidekeli; naliinua macho yangu, nikatazama, na kumbe, Mtu aliyevikwa nguo za kitani, viuno Vyake vimefungwa dhahabu safi ya Ufazi; mwili Wake pia ulikuwa kama zabarajadi safi, na uso Wake mfano wa umeme, na macho Yake kama taa za moto, na mikono Yake na miguu Yake rangi yake kama shaba iliyosuguliwa sana, na sauti ya maneno Yake kama sauti ya umati wa watu."*** (Danieli 10:2–6). **{SLsw 49.2}**

Maelezo haya yanafanana na yale yaliyotolewa na Yohana Kristo alipofunuliwa kwake katika kisiwa cha Patmo. Hakuna mwingine aliyemtokea Danieli isipokuwa Mwana wa Mungu. Bwana wetu alikuja pamoja na mjumbe mwingine wa mbinguni ili kumfundisha Danieli mambo ambayo yangetukia katika siku za mwisho. **{SLsw 49.3}**

Kweli kuu zilizofunuliwa na Mkombozi wa ulimwengu zimekusudiwa kwa wale wanaoutafuta Ukweli kama hazina zilizofichwa. Danieli alikuwa mzee. Maisha yake yalikuwa yamepita katikati ya mvuto wa ikulu ya kipagani, na akili yake ilikuwa imelemewa na mambo ya utawala wa milki kubwa. Hata hivyo, aliacha mambo hayo yote kando ili kuinyenyekeza nafsi yake mbele za Mungu na kutafuta kujua makusudi ya Yeye Aliye Juu. Na kwa kujibu maombi yake, nuru kutoka katika makao ya mbinguni ilifunuliwa kwa ajili ya wale ambao wangeishi katika siku za mwisho. Basi, sisi tunapaswa kumtafuta Mungu kwa bidii kubwa kiasi gani, ili afungue ufahamu wetu na kutuwezesha kuelewa Kweli tunazofunuliwa kutoka Mbinguni! **{SLsw 50.1}**

"Nami, Danieli, nikaona maono haya peke yangu; maana wale watu waliokuwa pamoja nami hawakuyaona maono haya; lakini tetemeko kuu liliwashika, hata wakakimbia ili kujificha. Basi nikaachwa peke yangu, nikaona maono haya makubwa, wala hazikubaki nguvu ndani yangu; maana uzuri wangu uligeuzwa ndani yangu kuwa uharibifu, wala sikusaziwa nguvu." (mistari ya 7, 8). Wote waliotakaswa kweli watakuwa na uzoefu unaofanana na huu. Kadiri wanavyopata mtazamo ulio wazi zaidi kuhusu ukuu,

utukufu, na ukamilifu wa Kristo, ndivyo watakavyoona kwa uwazi zaidi udhaifu na kutokamilika kwao wenyewe. Hawatakuwa na mwelekeo wa kudai kuwa wana tabia isiyo na dhambi; yale ambayo yalionekana kuwa mema na mazuri ndani yao, yakilinganishwa na usafi na utukufu wa Kristo, yataonekana tu kuwa yasiyostahili na yenye uharibifu tu. Ni wanadamu wanapokuwa wametengana na Mungu, na wanapokuwa na uelewa usio dhahiri kuhusu Kristo, ndipo wanaposema, “Mimi sina dhambi; nimetakaswa.” **{SLsw 50.2}**

Sasa Gabrieli alimtokea nabii huyo, akamwambia: ***“Ee Danielii, mtu upendwaye sana, yafahamu Maneno nikuambiayo, ukasimame kiwima-wima; maana kwako nimetumwa sasa. Na aliponiambia neno hili, nalisimama nikitetemeka. Ndipo akaniambia, Usiogope, Danieli; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako.”*** (mistari ya 11, 12). **{SLsw 51.1}**

Heshima ya Kifalme kwa Danieli

Ni heshima kubwa kama nini anayopewa Danieli na Mtukufu wa Mbinguni! Bwana Anamtia moyo mtumishi

Wake aliyekuwa akitetemeka na kumhakikishia kwamba sala yake ilikuwa imesikiwa Mbinguni. Kwa kujibu ombi hilo la ari na bidii, malaika Gabrieli alitumwa kugusa moyo wa mfalme wa Uajemi. Mfalme huyo wa himaya alikuwa ameupinga msukumo wa Roho wa Mungu kwa muda wote wa majuma matatu ambayo Danieli alikuwa akifunga na kusali; lakini Mkuu wa Mbinguni, Malaika Mkuu Mikaeli, alitumwa kuugeuza moyo wa mfalme huyo mkaidi ili mfalme achukue hatua thabiti ya kujibu sala ya Danieli. **{SLsw 51.2}**

"Na alipokwisha kusema nami maneno hayo, nikauelekeza uso wangu chini, nikawa bubu. Na kumbe, mmoja mfano wa wanadamu akanigusa midomo yangu; ndipo nikafumbua kinywa changu, nikanena, nikamwambia yeye aliyesimama karibu nami, Ee Bwana wangu, kwa sababu ya maono haya huzuni zangu zimenipata tena; hata sikusaziwa nguvu. Maana, mtumishi wa Bwana wangu huyu atawezaje kusema na Bwana wangu huyu? Kwa maana kwangu mimi, mara hazikusalia nguvu ndani yangu, wala pumzi haikusalia ndani yangu. Kisha mmoja mfano wa mwanadamu akanigusa tena, akanitia nguvu. Akasema, Ee mtu upendwaye sana, usiogope; amani na iwe kwako, uwe na nguvu, naam, uwe na nguvu. Aliposema nami

nikapata nguvu, nikasema, Ee Bwana wangu, na aseme Bwana wangu; kwa maana umenitia nguvu.” (mistari ya 15–19). Utukufu wa Mungu uliofunuliwa kwa Danieli ulikuwa mkuu sana hivi kwamba hakuweza kustahimili kuuona. Ndipo mjumbe wa Mbinguni akaufunika mwangaza wa uwepo Wake na akamtokea nabii huyo kama ***“Mmoja mfano wa Mwana wa wanadamu”*** (mstari wa 16). Kwa uwezo wa Kiungu, alimtia nguvu mtu huyu mwadilifu na mwenye imani ili aweze kuusikia ujumbe aliotumwa kutoka kwa Mungu. **{SLsw 51.3}**

Danieli alikuwa mtumishi aliyejitoa wakfu kwa Yeye Aliye Juu. Maisha yake marefu yalijazwa na matendo ya bora na ya kiungwana ya utumishi kwa Bwana wake. Usafi wa tabia yake na uaminifu wake usioyumba vililingana tu na unyenyekevu wa moyo wake na toba yake ya Kweli mbele za Mungu. Tunarudia kusema: Maisha ya Danieli ni kielelezo kilichoongozwa na Mungu cha utakaso wa Kweli. **{SLsw 52.1}**

SURA YA 7—TABIA YA YOHANA

Mtume Yohana alijulikana miongoni mwa ndugu zake kama “mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda.” Ingawa hakuwa mwoga, dhaifu, wala mwenye kusitasita hata kidogo katika tabia yake, alikuwa na tabia ya upole na moyo wenye uchangamfu na upendo. Inaonekana kwamba, kwa namna ya pekee sana, alifurahia urafiki wa Kristo, naye akapokea ishara nyingi za imani na upendo wa Mwokozi kwake. Alikuwa miongoni mwa wale watatu walioruhusiwa kushuhudia utukufu wa Kristo juu ya mlima wa kugeuka sura, pamoja na uchungu Wake huko Gethsemane; na katika saa zile za mwisho za maumivu Yake msalabani, Bwana wetu alimkabidhi Yohana jukumu la kumtunza mama Yake. **{SLsw 53.1}**

Yohana alijibu upendo wa Mwokozi kwa nguvu zote za ibada yake yenye shauku. Yohana alishikamana na Kristo kama vile mzabibu unavyoshikamana na nguzo

imara. Kwa ajili ya Bwana wake, alikabiliana kwa ujasiri na hatari za ukumbi wa hukumu na akabaki karibu na msalaba; na aliposikia habari kwamba Kristo amefufuka, aliharakisha kwenda kaburini kwa ari kubwa, hata akamtangulia Petro aliyekuwa na msukumo mkubwa. **{SLsw 53.2}**

Upendo wa Yohana kwa Bwana wake haukuwa urafiki wa kibinadamu tu, bali ulikuwa upendo wa mwenye dhambi aliyetubu, aliyekuwa akitambua kwamba amekombolewa kwa damu ya thamani ya Kristo. Alihesabu kuwa heshima kuu zaidi kufanya kazi na kuteseka katika utumishi wa Bwana wake. Upendo wake kwa Yesu ulimwongoza kuwapenda wote ambao Kristo aliwafia. Imani yake na dini yake ilikuwa ya vitendo-utendaji. Alitambua kwamba kumpenda Mungu hudhihirishwa kwa kuwapenda watoto Wake. Mara kwa mara alisikika akisema: ***"Wapenzi, ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana."*** (1 Yohana 4:11). ***"Sisi twampenda kwa sababu Yeye alitupenda sisi kwanza. Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona."*** (mistari ya 19, 20). Maisha ya mtume huyo yalikuwa

katika upatano na mafundisho yake. Upendo uliowaka moyoni mwake kwa Kristo ulimchochea kufanya kazi kwa bidii kubwa na bila kuchoka kwa ajili ya wanadamu wenzake, hasa kwa ajili ya ndugu zake katika kanisa la Kikristo. Alikuwa mhubiri mwenye nguvu, mwenye bidii na aliyejitoa kwa moyo wote-dhati; na maneno yake yalikuwa na nguvu kubwa ya kushawishi na kusadikisha. **{SLsw 53.3}**

Kiumbe Kipya Kupitia Neema

Upendo wa karibu na kujitoa bila ubinafsi uliodhihirishwa katika maisha na tabia ya Yohana unatoa mafundisho yenye thamani isiyoweza kupimika kwa kanisa la Kikristo. Wengine wanaweza kumwona kana kwamba alikuwa na upendo huo bila kutegemea neema ya Mungu; lakini kwa asili, Yohana alikuwa na kasoro kubwa za tabia; alikuwa mwenye kiburi na tamaa ya ukuu, na alikuwa mwepesi wa kuchukizwa alipotendewa kwa dharau au kudhulumiwa au kuumizwa. **{SLsw 54.1}**

Kina na ari ya upendo wa Yohana kwa Bwana wake havikuwa chanzo cha upendo wa Kristo kwake, bali vilikuwa matokeo ya upendo huo. Yohana alitamani kuwa kama Yesu, na chini ya ushawishi wa upendo wa Kristo unaobadilisha, akawa mpole na mnyenyekevu wa moyo.

Ubinafsi wake ulifichwa ndani ya Kristo**.** Aliunganishwa kwa karibu na Mzabibu ulio Hai, na hivyo akawa mshirika wa tabia ya kimungu. Hayo ndiyo matokeo ya kudumu ya ushirika na Kristo. Huu ndio utakaso wa Kweli. **{SLsw 54.2}**

Huenda mtu akawa na kasoro kubwa zinazoonekana katika tabia yake; hata hivyo, anapokuwa mwanafunzi wa kweli wa Yesu, nguvu ya neema ya Mungu humfanya kuwa kiumbe kipya. Upendo wa Kristo humbadilisha na kumtakasa. Lakini watu wanapodai kuwa ni Wakristo, na dini yao haiwafanyi kuwa wanaume na wanawake bora katika mahusiano yote ya maisha—yaani, kuwa wawakilishi hai wa Kristo katika hulka na tabia—hao sio Wake. **{SLsw 55.1}**

Mafundisho katika Kujenga Tabia

Wakati mmoja, Yohana alibishana na baadhi ya ndugu zake kuhusu ni nani kati yao angehesabiwa kuwa mkuu zaidi. Hawakuwa na nia ya kumfanya Bwana wao ayasikie maneno yao; lakini Yesu aliisoma mioyo yao, akatumia fursa hiyo kuwafundisha wanafunzi Wake somo la unyenyekevu. Somo hilo halikuwa kwa ajili ya kikundi kidogo tu kilichosikiliza maneno Yake, bali liliandikwa pia kwa manufaa ya wafuasi Wake wote hadi mwisho wa

wakati. ***"Akaketi chini, akawaita wale Thenashara akawaambia, Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote."*** (Marko 9:35). **{SLsw 55.2}**

Wale walio na roho ya Kristo hawatakuwa na tamaa ya ukuu wa kushikilia nafasi iliyo juu ya ndugu zao. Ni wale wanaojiona kuwa wadogo machoni pao wenyewe ndio watakaohesabiwa kuwa wakuu machoni pa Mungu. ***"Akatwaa kitoto, akamweka katikati yao, akamkumbatia, akawaambia, Mtu akimpokea mtoto mmoja wa namna hii kwa Jina Langu, anipokea Mimi; na mtu akinipokea Mimi, humpokea, si Mimi, bali yeye aliyenituma."*** (mistari ya 36, 37). **{SLsw 55.3}**

Ni somo la thamani iliyoje kwa wafuasi wote wa Kristo! Wale wanaopuuza wajibu wa maisha unaokutana nao moja kwa moja katika njia yao, na wanaopuuza kuonyesha rehema, fadhili, adabu na upendo hata kwa mtoto mdogo, wanampuuza Kristo. Yohana alitambua uzito wa somo hili na akanufaika nalo. **{SLsw 56.1}**

Katika tukio jingine, Yohana na ndugu yake Yakobo walimwona mtu akiwatoa pepo kwa Jina la Yesu. Kwa sababu mtu huyo hakuwa amejiunga mara moja na kundi lao, waliamua kwamba hakuwa na haki ya kufanya kazi

hiyo, na kwa hiyo wakamkataza. Kwa unyofu wa moyo, Yohana alimweleza Bwana wake jambo hilo. Yesu akasema, ***"Msimkataze, kwa kuwa hakuna mtu atakayefanya mwujiza kwa Jina Langu akaweza mara kuninenea mabaya; kwa sababu asiye kinyume chetu, yu upande wetu."*** (mistari ya 39, 40). **{SLsw 56.2}**

Tena, Yakobo na Yohana, kwa kumtumia mama yao, waliwasilisha ombi kwamba waruhusiwe kushika nafasi za juu kabisa za heshima katika ufalme wa Kristo. Mwokozi akawajibu, ***"Hamjui mnaloliomba"*** (Marko 10:38). Ni kwa kiasi gani wengi wetu hatuelewi maana halisi ya maombi yetu! Yesu alijua kwamba utukufu huo ungepatikana kwa gharama ya dhabihu isiyo na kifani, wakati Yeye, ***"kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu."*** (Waebrania 12:2). Furaha hiyo ilikuwa ni kuona roho zikiokolewa kwa njia ya kujinyenyekeza Kwake, uchungu Wake na kumwagwa kwa damu Yake. **{SLsw 56.3}**

Huo ndio ulikuwa utukufu ambao Kristo angeupokea, na ambao wanafunzi hawa wawili waliomba waruhusiwe kushiriki. Yesu akawauliza, **"Je, Mwaweza kunywea kikombe ninyweacho mimi, au kubatizwa ubatizo**

nibatizwao Mimi? Nao wakasema, **"Twaweza"** (Marko 10:38, 39). **{SLsw 57.1}**

Ni kwa kiasi gani watu hawa hawakuelewa maana ya ubatizo huo! ***"Yesu akawaambia, Kikombe ninyweacho Mimi mtakinywea, na ubatizo nibatizwao Mimi mtabatizwa; lakini habari ya kuketi mkono Wangu wa kuume au mkono Wangu wa kushoto si Langu kuwapa, ila wao watapewa waliowekewa tayari."*** (mistari ya 39, 40). **{SLsw 57.2}**

Kiburi na Tamaa ya Ukuu Vyakemewa

Yesu alielewa nia zilizokuwa zimechochea ombi hilo, na hivyo akaukemea kiburi na tamaa ya ukuu iliyokuwa ndani ya wanafunzi hao wawili: ***"Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu anayetaka kuwa mkubwa kwenu, atakuwa mtumishi wenu, na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote. Kwa maana Mwana wa Adamu Naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi Yake iwe fidia ya wengi."*** (mistari ya 42–45). **{SLsw 57.3}**

Wakati mmoja, Kristo aliwatuma wajumbe watangulie mbele Yake ili kwenda katika kijiji kimoja cha Wasamaria, kuwaomba watu hao waandae chakula kwa ajili Yake na wanafunzi Wake ili waburudishwe. Lakini Mwokozi alipokikaribia kijiji hicho, alionekana kana kwamba alikuwa akielekea Yerusalemu. Jambo hilo liliamsha uadui wa Wasamaria, na badala ya kutuma wajumbe kumwalika, au hata kumsihi akae pamoja nao, walimnyima ukarimu ambao wangemwonyesha hata msafiri wa kawaida. Yesu hamlazimishi mtu yeyote kumpokea, nao Wasamaria wakapoteza baraka ambayo wangepokea kama wangemwomba awe mgeni wao. **{SLsw 57.4}**

Tunaweza kushangazwa na kutendewa huku kwa kukosa adabu kwa Mtukufu wa Mbinguni; lakini ni mara ngapi sisi tunaodai kuwa wafuasi wa Kristo tunakuwa na hatia ya kumpuuza kwa namna hiyo hiyo? Je, tunamsihi Yesu akae ndani ya mioyo yetu na katika nyumba zetu? Yeye amejaa upendo, neema na baraka, Naye Yuko tayari kutupatia zawadi hizo; lakini, kama Wasamaria, mara nyingi tunaridhika kuishi bila baraka hizo. **{SLsw 58.1}**

Wanafunzi walijua kusudi la Kristo la kuwabariki Wasamaria kwa uwepo Wake; na walipoona ubaridi, wivu

na kutomheshimu Bwana wao, walijawa na mshangao na ghadhabu. Yakobo na Yohana walichochewa na mihemko zaidi. Kwao, kutendwa hivyo kwa Yeye waliyemheshimu sana kulionekana kuwa kosa kubwa sana ambalo halikupaswa kuachwa bila adhabu ya mara moja. Kwa shauku yao kubwa, wakasema, ***"Bwana, wataka tuamuru moto ushuke kutoka mbinguni, uwateketeze, kama Eliya alivyofanya?"*** (Luka 9:54), wakirejelea kuangamizwa kwa maakida wa Washami na vikosi vyao waliotumwa kumkamata nabii Eliya. **{SLsw 58.2}**

Yesu aliwakemea wanafunzi Wake, akisema, **"Akasema, Hamjui ni roho ya namna gani mliyo nayo. Kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa."** (mistari ya 55, 56). Yohana na wanafunzi wenzake walikuwa katika shule ambayo Kristo alikuwa Mwalimu wao. Wale waliokuwa tayari kuona kasoro zao wenyewe na waliokuwa na shauku ya kuboresha tabia zao walikuwa na fursa nyingi za kufanya hivyo. Yohana alithamini kila somo na daima alijitahidi kuyafanya maisha yake yapatane na Kielelezo cha Kimungu. Mafundisho ya Yesu, yaliyosisitiza kwamba upole, utu wema, unyenyekevu na upendo ni mambo muhimu kwa kukua katika neema na kuwa tayari kwa ajili ya kazi Yake, yalikuwa ya thamani kubwa sana

kwa Yohana. Mafundisho hayo yanaelekezwa kwetu sisi mmoja mmoja na kama ndugu katika kanisa, kama vile yalivyoelekezwa kwa wanafunzi wa kwanza wa Kristo. **{SLsw 59.1}**

Yohana na Yuda

Somo lenye mafundisho makubwa linaweza kupatikana katika tofauti ya wazi kati ya tabia ya Yohana na ile ya Yuda. Yohana alikuwa kielelezo hai cha utakaso. Kwa upande mwingine, Yuda alikuwa na mfano wa utauwa, ingawa tabia yake ilikuwa ya kishetani zaidi kuliko ya Kiungu. Alidai kuwa mwanafunzi wa Kristo, lakini kwa maneno na matendo yake alimkana. **{SLsw 59.2}**

Yuda alikuwa na fursa zilezile za thamani ambazo Yohana alikuwa nazo za kujifunza na kumwiga Kielelezo. Alisikiliza mafundisho ya Kristo, na tabia yake ingeweza kubadilishwa kwa neema ya Mungu. Lakini wakati Yohana alipokuwa akipambana kwa bidii dhidi ya kasoro zake mwenyewe na kujitahidi kufanana na Kristo, Yuda alikuwa akikiuka dhamiri yake, akijisalimisha kwa majaribu, na kujizoesha kutokuwa mwaminifu, mazoea ambayo yangembadilisha na kumfanya afanane na Shetani. **{SLsw 59.3}**

Wanafunzi hawa wawili wanawakilisha ulimwengu wa Kikristo. Wote wanadai kuwa wafuasi wa Kristo; lakini wakati kundi moja linatembea kwa unyenyekevu na upole, likijifunza kutoka kwa Yesu, kundi jingine linaonyesha kwamba si watendaji wa Neno, bali wasikilizaji tu. Kundi la kwanza linatakaswa kwa njia ya Kweli; kundi la pili halijui lolote kuhusu nguvu ya neema ya Mungu inayobadilisha. Kundi la kwanza huifia nafsi kila siku na kuushinda dhambi; la pili hujifurahisha na kujiendekeza katika tamaa zao wenyewe na kuwa watumwa wa Shetani. **{SLsw 60.1}**

SURA YA 8—HUDUMA YA YOHANA

Mtume Yohana alitumia miaka ya mwanzo ya maisha yake miongoni mwa wavuvi wa kawaida, wasio na elimu ya darasani, huko Galilaya. Hakupata mafunzo ya shuleni; lakini kwa kushirikiana na Kristo, Mwalimu Mkuu, alipata elimu ya juu kabisa ambayo mwanadamu mwenye kufa anaweza kuipokea. Alikunywa kwa shauku katika chemchemi ya hekima, kisha akatafuta kuwaongoza wengine kwenye *"kisima cha maji kinachobubujika uzima wa milele"* (Yohana 4:14). Usahili wa maneno yake, nguvu kuu ya zile Kweli alizotangaza, na ari ya kiroho iliyodhihirisha mafundisho yake vilimfungulia njia

kwa watu wa tabaka zote. Hata hivyo, hata waumini hawakuweza kuelewa kikamilifu mafumbo matakatifu ya Ukweli wa Mungu yaliyofunuliwa katika hotuba zake. Alionekana kuwa amejazwa Roho Mtakatifu daima. Alijitahidi kuinua mawazo ya watu ili waweze kufahamu mambo yasiyoonekana. Hekima iliyodhihirika katika maneno yake ilisababisha maneno hayo kudondoka kama umande, yakilainisha na kuituliza nafsi. **{SLsw 61.1}**

Baada ya Kristo kupaa, Yohana alijitokeza kuwa mtenda kazi mwaminifu na mwenye bidii kwa ajili ya Bwana wake. Pamoja na wengine, alishiriki katika kumwagwa kwa Roho siku ya Pentekoste, na kwa bidii na nguvu mpya aliendelea kuwaambia watu Maneno ya uzima. Alitishiwa kufungwa na kuuawa, lakini hakutishwa wala kurudi nyuma. **{SLsw 61.2}**

Watu wa tabaka zote walijitokeza kusikiliza mahubiri ya mitume, nao waliponywa magonjwa yao kwa jina la Yesu—jina lililochukiwa sana miongoni mwa Wayahudi. Makuhani na watawala walijawa na ghadhabu na msukosuko mkubwa katika upinzani wao walipoona kwamba wagonjwa walikuwa wakiponywa na kwamba Yesu alikuwa akitukuzwa kuwa Mkuu wa uzima. Waliogopa kwamba hivi karibuni ulimwengu wote

ungemwamini, na kisha wangetuhumiwa kuwa wamemuua Mponyaji Mkuu. Lakini kadiri walivyozidisha juhudi zao za kuzuia mwamko huo, ndivyo watu wengi zaidi walivyomwamini Yesu na kuyaacha mafundisho ya Waandishi na Mafarisayo. Wakiwa wamejawa na ghadhabu, wakawakamata Petro na Yohana na kuwatupa katika gereza la kawaida. Lakini malaika wa Bwana, wakati wa usiku, akafungua milango ya gereza, akawatoa, na kusema, ***"Enendeni mkasimame hekaluni mkawaambie watu maneno yote ya Uzima huu."*** (Matendo 5:20). **{SLsw 62.1}**

Kwa uaminifu na bidii, Yohana alitoa ushuhuda kwa ajili ya Bwana wake kila alipokuwa na nafasi inayofaa. Aliona kwamba nyakati hizo zilikuwa zimejaa hatari kwa kanisa. Udanganyifu wa kishetani ulikuwa umeenea kila mahali. Mawazo ya watu yalikuwa yakipotelea katika mapito ya mashaka na mafundisho ya Biblia yenye udanganyifu (deceptive doctrines). Baadhi ya watu waliojifanya kuwa waaminifu kwa kazi ya Mungu walikuwa wadanganyifu. Walimkana Kristo na Injili Yake, wakaingiza mafundisho potovu yenye kuangamiza, na kuishi katika uasi dhidi ya sheria ya Mungu. **{SLsw 62.2}**

Mada Pendwa ya Yohana

Mada aliyopenda sana Yohana ilikuwa upendo usio na kikomo wa Kristo. Alimwamini Mungu kama mtoto anavyomwamini baba Mwenye fadhili na huruma. Alielewa tabia na kazi ya Yesu; na alipowaona ndugu zake Wayahudi wakijaribu kuchechemea kuitafuta njia bila hata miale ya Jua la Haki kuwaangazia katika njia yao, alitamani kumtangaza Kristo kwao, Yeye aliye Nuru ya ulimwengu. **{SLsw62.3}**

Mtume huyo mwaminifu aliona kwamba upofu wao, kiburi, ushirikina, na kutokuyajua kwao Maandiko vilikuwa vikifunga nafsi zao kwa minyororo ambayo isingevunjwa kamwe. Ubaguzi na chuki dhidi ya Kristo, walizoshikilia kwa ukaidi, vilikuwa vikileta maangamizi juu ya taifa lao na kuharibu matumaini yao ya uzima wa milele. Lakini Yohana aliendelea kuwaonyesha Kristo kuwa njia pekee ya wokovu. Ushahidi kwamba Yesu wa Nazareti alikuwa Masihi ulikuwa wazi sana kiasi kwamba Yohana anatangaza kwamba hakuna mtu anayehitaji kutembea katika giza la upotovu wakati nuru kama hiyo inapotolewa kwake. **{SLsw 63.1}**

Akiwa na Huzuni kwa Sababu ya Makosa Yenye Sumu

Yohana aliishi kuona Injili ya Kristo ikihubiriwa kila mahali, na maelfu ya watu wakiyakubali mafundisho yake kwa shauku. Lakini alijawa na huzuni alipoona makosa yenye sumu yakianza kuingia ndani ya kanisa taratibu. Baadhi ya wale waliompokea Kristo walidai kwamba upendo Wake uliwaweka huru wasiitii sheria ya Mungu. Kwa upande mwingine, wengi walifundisha kwamba sheria inapaswa kushikwa kwa kufuata maandishi yake, pamoja na desturi na sherehe zote za Kiyahudi, na kwamba hayo yalitosha kwa wokovu bila damu ya Kristo. Walidai kwamba Kristo alikuwa mtu mwema, kama mitume, lakini walikana Uungu Wake. Yohana aliona hatari ambazo kanisa lingekabili iwapo lingekubali mawazo hayo, naye akakabiliana nayo kwa haraka na kwa uthabiti. Akamwandikia mwanamke mmoja mwenye kuheshimika sana, aliyekuwa mshiriki wa kazi ya Injili, mwenye sifa njema na ushawishi mkubwa: **{SLsw 63.2}**

"Kwa maana wadanganyifu wengi wametokea duniani, wasiokiri ya kuwa Yesu Kristo Yuaja katika mwili. Huyo ndiye yule mdanganyifu na mpinga Kristo. Jiangalieni nafsi zenu msiyapoteze mliyoyatenda, bali

mpokee thawabu timilifu. Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia. Mtu akija kwenu, naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu. Maana yeye ampaye salamu azishiriki kazi zake mbovu." (2 Yohana 7–11). **{SL 64.1}**

Yohana hakuendeleza kazi yake bila kukumbana na vikwazo vikubwa. Shetani hakukaa kivivu bila kazi ya uovu. Aliwachochea watu waovu ili kuyakatisha maisha yenye manufaa ya mtu huyu wa Mungu, lakini malaika watakatifu walimlinda dhidi ya mashambulizi yao. Yohana alipaswa kusimama kama shahidi mwaminifu wa Kristo. Kanisa, lilipokuwa katika hatari, lilihitaji ushuhuda wake. **{SLsw 64.2}**

Kwa upotoshaji na uwongo, mawakala wa Shetani walikuwa wamejaribu kuchochea upinzani dhidi ya Yohana na dhidi ya mafundisho ya Kristo. Kwa sababu hiyo, migawanyiko na mafundisho potovu vilikuwa vikilihatarisha kanisa. Yohana alikabiliana na makosa hayo bila kuyumba. Aliwazibia njia wapinzani wa Ukweli. Aliandika na kushauri kwamba viongozi wa mafundisho hayo potovu wasipewe hata dalili ndogo ya

kutiwa moyo katika mafundisho hayo. Katika siku hizi, kuna maovu yanayofanana na yale yaliyolitishia ustawi wa kanisa la kwanza, na mafundisho ya mtume kuhusu mambo hayo yanapaswa kuzingatiwa kwa makini. “Ni lazima uwe na upendo,” ndicho kilio kinachosikika kila mahali, hasa kutoka kwa wale wanaodai kuwa wametakaswa. Lakini upendo ni safi sana kiasi kwamba hauwezi kufunika dhambi ambayo haijaungamwa. Mafundisho ya Yohana ni muhimu kwa wale wanaoishi katikati ya hatari za siku za mwisho. Alikuwa ameshirikiana kwa karibu sana na Kristo, alikuwa amesikiliza mafundisho Yake na kushuhudia miujiza Yake yenye nguvu. Alitoa ushuhuda wenye ushawishi mkubwa, ulioufanya uwongo wa maadui wa Kristo ukose nguvu. **{SLsw 64.3}**

Hakuna Mapatano na Dhambi

Yohana alifurahia baraka ya utakaso wa Kweli. Lakini zingatia kwamba mtume huyo hajidai kuwa hana dhambi; anajitahidi kufikia ukamilifu kwa kutembea katika nuru ya uso wa Mungu. Anashuhudia kwamba mtu anayesema anamjua Mungu, lakini hazishiki amri Zake,

anathibitisha kwamba dai lake ni la uongo. **“Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala Kweli haimo ndani yake.”** (1 Yohana 2:4). Katika kizazi hiki kinachojivunia uhuru mpana wa mawazo na uvumilivu, maneno haya yangetajwa kuwa ya ushupavu wa kidini au kupitiliza. Lakini mtume anafundisha kwamba, ingawa tunapaswa kudhihirisha adabu ya Kikristo, tuna haki ya kuiita dhambi na wenye dhambi kwa majina yao halisi—na kwamba kufanya hivyo kunapatana na upendo wa Kweli. Ingawa tunapaswa kuwapenda wale ambao Kristo aliwafia na kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wao, hatupaswi kufanya mapatano na dhambi. Hatupaswi kuungana na waasi na kuliita jambo hilo upendo. Mungu anawataka watu Wake katika kizazi hiki wasimame, kama Yohana alivyofanya katika wakati wake, bila kuyumba kwa ajili ya haki, wakipinga makosa yanayoharibu nafsi. **{SLsw 65.1}**

Hakuna Utakaso Bila Utii

Nimekutana na watu wengi waliodai kuishi bila dhambi. Lakini walipopimwa kwa Neno la Mungu, watu hao walionekana kuwa wavunjaji wa sheria Yake Bwana takatifu kwa wazi kabisa. Ushahidi ulio wazi kabisa wa

kudumu kwa Amri ya Nne na wa mamlaka yake ya lazima ulishindwa kuamsha dhamiri zao. Hawakuweza kupinga madai ya Mungu, lakini walithubutu kutoa visingizio vya kuendelea kuivunja Sabato. Walidai kuwa wametakaswa, na kwamba wanamtumikia Mungu siku zote za juma. Walisema kwamba watu wengi wema hawakuitunza Sabato. Kama watu wangekuwa wametakaswa, wasingepatwa na hukumu yoyote kwa kutokuitunza. Mungu alikuwa Mwenye rehema sana kiasi cha kutowaadhibu kwa kutokuitunza siku ya saba. Walidai kwamba wangeonekana kuwa watu wa pekee katika jamii ikiwa wangeitunza Sabato, na kwamba wasingekuwa na ushawishi wowote ulimwenguni. Pia walidai kwamba walipaswa kujitiisha kwa mamlaka zilizopo. **{SLsw 66.1}**

Mwanamke mmoja huko New Hampshire alitoa ushuhuda wake katika mkutano wa hadhara kwamba neema ya Mungu ilikuwa ikitawala moyoni mwake na kwamba alikuwa wa Bwana kikamilifu. Kisha akaeleza imani yake kwamba watu hawa walikuwa wakifanya mema mengi kwa kuwaamsha wenye dhambi watambue hatari yao. Alisema, “Sabato ambayo watu hawa wanatufundisha ndiyo Sabato pekee ya Biblia”; kisha akaeleza kwamba akili yake ilikuwa imeshughulishwa

sana na jambo hilo. Aliona majaribu makubwa mbele yake ambayo alipaswa kukabiliana nayo ikiwa angeitunza siku ya saba. Siku iliyofuata alikuja kwenye mkutano na tena akatoa ushuhuda wake, akisema kwamba alikuwa amemwomba Bwana ikiwa alipaswa kuitunza Sabato, naye alikuwa amemwambia kwamba hakupaswa kuitunza. Sasa akili yake ilikuwa imetulia kuhusu jambo hilo. Kisha akatoa himizo lenye nguvu sana kwa wote wafikie upendo mkamilifu wa Yesu, ambamo hakuna hukumu juu ya nafsi. **{SLsw 66.2}**

Mwanamke huyu hakuwa na utakaso wa kweli. Si Mungu aliyemwambia kwamba angeweza kutakaswa huku akiishi katika kutotii mojawapo ya amri Zake zilizo wazi. Sheria ya Mungu ni takatifu, na hakuna mtu anayeweza kuivunja bila kuadhibiwa. Yule aliyemwambia kwamba angeweza kuendelea kuivunja sheria ya Mungu na bado asiwe na dhambi alikuwa mkuu wa nguvu za giza—yuleyule aliyemwambia Hawa huko Edeni, kupitia nyoka, ***"Hakika hamtakufa"*** (Mwanzo 3:4). Hawa alijidanganya kwamba Mungu alikuwa mwema sana kiasi cha kutomwadhibu kwa kutotii amri Yake iliyo wazi. Hoja hiyo ya ujanja na udanganyifu inatumiwa na maelfu ya watu kama kisingizio cha kutotii Amri ya Nne. Wale walio na nia ya Kristo watazitunza amri zote za Mungu,

bila kujali mazingira. Mtukufu wa Mbinguni anasema, ***"Kama vile Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu"*** (Yohana 15:10). **{SLsw 67.1}**

Adamu na Hawa walithubutu kuyavunja matakwa ya Bwana, na matokeo mabaya ya dhambi yao yanapaswa kuwa onyo kwetu tusifuate mfano wao wa kutotii. Kristo aliwaombea wanafunzi Wake kwa Maneno haya: ***"Uwatakase kwa ile Kweli; Neno Lako ndiyo Kweli"*** (Yohana 17:17). Hakuna utakaso wa kweli isipokuwa kupitia utii kwa ile kweli. Wale wanaompenda Mungu kwa moyo wote watazipenda pia amri Zake zote. Moyo uliotakaswa unapatana na maagizo ya sheria ya Mungu; kwa maana maagizo hayo ni matakatifu, ya haki, na mema. **{SLsw 67.2}**

Mungu Hajabadilika

Tabia ya Mungu haijabadilika. Yeye ni Mungu Yule Yule Mwenye wivu leo kama alivyokuwa wakati alipotoa sheria Yake juu ya Mlima Sinai na kuiandika kwa kidole Chake mwenyewe juu ya mbao za mawe. Wale wanaokanyaga sheria takatifu ya Mungu wanaweza kusema, *"Mimi nimetakaswa";* lakini kutakaswa kweli na kudai kuwa umetakaswa ni mambo mawili tofauti. **{SLsw 68.1}**

Agano Jipya halijabadilisha sheria ya Mungu. Utakatifu wa Sabato ya Amri ya Nne umewekwa kwa uthabiti uleule kama kiti cha enzi cha Yehova. Yohana anaandika: **“Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi. Nanyi mnajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani Yake. Kila akaaye ndani Yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona Yeye, wala hakumtambua.”** (1 Yohana 3:4–6). Tumeambiwa kuwaona kwa mtazamo uleule aliokuwa nao mwanafunzi huyo mpendwa wale wanaodai kukaa ndani ya Kristo na kutakaswa, huku wakiishi katika uasi dhidi ya sheria ya Mungu. Yohana alikabiliana na kundi kama hilo ambalo nasi tunapaswa kukabiliana nalo. Alisema, ***“Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki; atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi.”*** (mistari ya 7, 8). Hapa mtume anazungumza kwa maneno yaliyo wazi, kama alivyoona jambo hilo lilivyohitaji. **{SLsw 68.2}**

Nyaraka za Yohana zimejaa roho ya upendo. Lakini anapokutana na watu wa kundi hilo wanaovunja sheria ya Mungu huku wakidai kwamba wanaishi bila dhambi,

hasiti kuwaonya kuhusu udanganyifu wao wa kutisha. ***"Tukisema ya kwamba twashirikiana Naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo Kweli; bali tukienenda nuruni, kama Yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu Yake Yesu, Mwana Wake, yatusafisha dhambi yote. Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala Kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala Neno Lake halimo mwetu."*** (1 Yohana 1:6–10). **{SLsw 68.3}**

SURA YA 9—YOHANA UHAMISHONI

Mafanikio makubwa yaliyotokana na mahubiri ya Injili yaliyofanywa na mitume pamoja na watenda kazi wenzao yalizidisha chuki ya maadui wa Kristo. Walifanya kila juhudi kuzuia kuenea kwa juhudi zote za Injili hiyo,

na hatimaye wakafanikiwa kuishawishi mamlaka ya mfalme wa Roma itumike dhidi ya Wakristo. Kisha yakafuata mateso makali, ambayo katika hayo wafuasi wengi wa Kristo waliuawa. Mtume Yohana sasa alikuwa mzee, lakini aliendelea kuhubiri mafundisho ya Kristo kwa bidii kubwa na kwa mafanikio [Doctrine of Christ]. Alikuwa na ushuhuda wenye nguvu ambao wapinzani wake hawakuweza kuupinga, na ambao uliwatia moyo sana ndugu zake. **{SLsw 70.1}**

Imani ya Wakristo ilipoonekana kuyumba chini ya upinzani mkali ambao walilazimika kukabiliana nao, mtume alikuwa akiyarudia kwa heshima kuu, nguvu, na ufasaha maneno haya: "***Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la uzima; (na uzima huo ulidhihirika, nasi tumeona, tena twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uzima wa milele, uliokuwa kwa Baba, ukadhihirika kwetu); hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana Wake Yesu Kristo."*** (1 Yohana 1:1–3). **{SLsw 70.2}**

Chuki kali sana iliwashwa dhidi ya Yohana kwa sababu ya uaminifu wake usioyumba kwa kazi ya Kristo. Yeye ndiye aliyekuwa mwanafunzi wa mwisho aliyekuwa bado hai miongoni mwa wale waliokuwa na uhusiano wa karibu sana na Yesu, na maadui zake waliamua kwamba ushuhuda wake lazima unyamazishwe. Ikiwa wangefanikiwa kufanya hivyo, walifikiri kwamba mafundisho ya Kristo yasingeenea; na ikiwa angeadhibiwa vikali, huenda mafundisho hayo yangetoweka upesi duniani. Kwa hiyo Yohana aliitwa kwenda Roma ili kuhukumiwa kwa sababu ya imani yake. Mafundisho yake yalipotoshwa. Mashahidi wa uongo walimshtaki kuwa mchochezi, aliyekuwa akifundisha hadharani nadharia ambazo zingepindua taifa. **{SLsw 70.3}**

Mtume aliwasilisha imani yake kwa njia iliyo wazi na yenye kusadikisha, kwa unyenyekevu na unyoofu kiasi kwamba maneno yake yalikuwa na athari kubwa. Wasikilizaji wake walishangazwa na hekima na ufasaha wake. Lakini kadiri ushuhuda wake ulivyokuwa wenye kusadikisha zaidi, ndivyo chuki ya wale walioupinga Ukweli ilivyozidi kuwa kubwa. Mfalme wa himaya alijawa na ghadhabu, akalitukana Jina la Mungu na la Kristo. Hakuweza kupinga hoja za mtume wala kulingana na nguvu iliyoambatana na kutangazwa kwa Ukweli,

hivyo akaazimia kumnyamazisha mtetezi huyo mwaminifu wa Ukweli. **{SLsw 71.1}**

Shahidi wa Mungu Hakunyamazishwa

Hapa tunaona jinsi moyo unavyoweza kuwa mgumu mtu anapopinga kwa ukaidi makusudi ya Mungu. Maadui wa kanisa walikuwa wameazimia kudumisha kiburi na mamlaka yao mbele ya watu. Kwa amri ya mfalme, Yohana alihamishiwa katika kisiwa cha Patmo kama mtu aliyefukuzwa, akihukumiwa, kama anavyotuambia, **"kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo"** (Ufunuo 1:9). Lakini maadui wa Kristo walishindwa kabisa katika kusudi lao la kumnyamazisha shahidi Wake mwaminifu. Kutoka mahali pake pa uhamishoni, sauti ya mtume iliendelea kusikika, hata kufikia mwisho wa wakati, ikitangaza Kweli zenye kusisimua zaidi ambazo zimewahi kufunuliwa kwa wanadamu. **{SLsw 71.2}**

Patmo, kisiwa chenye miamba mikavu katika Bahari ya Aegean, kilikuwa kimechaguliwa na serikali ya Roma kuwa mahali pa kuwahamishia wahalifu. Lakini kwa mtumishi wa Mungu, makao hayo ya huzuni yakawa lango la mbinguni. Alitengwa na shughuli zenye pilikapilika za maisha na kazi ya utendaji kama mwinjilisti, lakini hakutengwa na uwepo wa Mungu.

Katika makao yake ya upweke, aliwasiliana na Bwana na aliweza kuwa na ushirika na Mfalme wa wafalme na kujifunza kwa undani zaidi udhihirisho wa nguvu za Mungu katika kitabu cha maumbile na katika kurasa za Maandiko yaliyovuviwa. Alifurahia kutafakari juu ya kazi kuu ya uumbaji na kustaajabia nguvu za Mbunifu wa Kimungu. Katika miaka ya awali, macho yake yalikuwa yamezoea kuona vilima vilivyofunikwa na miti, mabonde yenye majani mabichi, na tambarare zenye rutuba; na katika uzuri wote wa asili, alifurahia kufuatilia hekima na ustadi wa Muumba. Sasa alikuwa amezungukwa na mandhari ambayo kwa wengi yangeonekana kuwa ya huzuni na yasiyovutia. Lakini kwa Yohana ilikuwa tofauti. Aliweza kusoma mafundisho muhimu sana katika miamba ya pori na ukiwa, mafumbo ya vilindi vikuu vya bahari, na utukufu wa anga. Kwake, yote hayo yalikuwa na alama ya nguvu za Mungu na yalitangaza utukufu Wake. **{SLsw 72.1}**

Sauti ya Maumbile

Mtume aliona pande zote zilizomzunguka ambazo zilikuwa mashahidi wa Gharika iliyoifunika dunia kwa sababu wakazi wake walithubutu kuivunja sheria ya

Mungu. Miamba iliyotupwa juu kutoka vilindini mwa bahari kuu na kutoka ardhini kwa sababu ya maji yaliyofurika, ilimkumbusha kwa uhalisia mkubwa vitisho vya kumwagwa kwa ghadhabu hiyo kuu ya Mungu. **{SLsw 72.2}**

Lakini ingawa kila kitu kilichomzunguka chini kilionekana kuwa cha ukiwa na kisicho na rutuba, mbingu za buluu zilizotanda juu ya mtume huyo katika Patmo yenye upweke zilikuwa angavu na nzuri kama anga la Yerusalemu yake mpendwa. Mwanadamu akiitazama fahari ya mbingu wakati wa usiku na kutafakari kazi ya nguvu za Mungu katika majeshi ya nyota zilizomo humo, hujifunza somo kuhusu ukuu wa Muumba kwa kulinganisha na udogo wake mwenyewe. Ikiwa amekuwa akifurahia kukuza kiburi na kujiona kuwa wa maana kwa sababu ya utajiri, vipawa, au mvuto wake wa kibinafsi, na atoke usiku huo mzuri na kutazama mbingu zenye nyota, atajifunza kuunyenyekesha moyo wake wenye kiburi mbele za Yeye Asiye na ukomo. **{SLsw 73.1}**

Katika sauti ya maji mengi—vilindi vikiitana—nabii alisikia sauti ya Muumba. Bahari iliyochafuka kwa nguvu na kuchochewa na pepo zisizo na huruma iliwakilisha ghadhabu ya Mungu aliyekasirishwa. Mawimbi makuu,

katika msukosuko wao wa kutisha, yaliyokuwa yamezuiwa ndani ya mipaka iliyowekwa na mkono usioonekana, yalimwambia Yohana juu ya nguvu isiyo na kikomo inayoutawala vilindi vya bahari. Na kwa kulinganisha na hayo, aliona na kuhisi upumbavu wa wanadamu wanyonge wenye ukomo, ambao si kitu ila minyoo ya mavumbi, lakini hujivunia hekima na nguvu zao na kuigeuza mioyo yao dhidi ya Mtawala wa ulimwengu, kana kwamba Mungu ni kama wao kabisa. Jinsi kiburi cha mwanadamu kilivyo na upofu na kisicho na utashi! Saa moja tu ya baraka za Mungu, kupitia mwanga wa jua na mvua juu ya dunia, inaweza kubadili sura ya maumbile kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko mwanadamu, pamoja na maarifa yake yote anayojivunia na juhudi zake zote za kudumu, anavyoweza kutimiza katika maisha yake yote. **{SLsw 73.2}**

Katika mazingira ya kisiwa chake cha uhamishoni, nabii huyo aliyehamishwa alisoma udhihirisho wa nguvu za Mungu, na katika kazi zote za maumbile aliendelea kuwa na ushirika na Mungu wake. Hamu kuu kabisa ya nafsi ya kumtafuta Mungu, pamoja na maombi ya dhati kabisa, yalipaa kwenda mbinguni kutoka Patmo yenye miamba. Yohana alipoitazama ile miamba, alikumbushwa

kuhusu Kristo, Mwamba wa nguvu zake, ambaye katika kivuli Chake angeweza kujificha bila hofu. **{SLsw 74.1}**

Mtunza-Sabato

Siku ya Bwana iliyotajwa na Yohana ilikuwa Sabato, siku ambayo Yehova alipumzika baada ya kazi kuu ya uumbaji, na ambayo aliibariki na kuitakasa kwa sababu alipumzika siku hiyo. Yohana aliitunza Sabato kwa utakatifu uleule katika Kisiwa cha Patmo kama alivyofanya alipokuwa miongoni mwa watu, akihubiri katika siku hiyo. Miamba mikavu iliyomzunguka ilimkumbusha Yohana Horebu pale Sinai, yenye miamba, na jinsi Mungu aliponena nao huko kuhusu sheria Yake, akisema, ***"Ikumbuke siku ya Sabato uitakase"*** (Kutoka 20:8). **{SLsw 74.2}**

Mwana wa Mungu alinena na Musa kutoka kileleni mwa mlima. Mungu aliifanya miamba kuwa Patakatifu Pake. Hekalu Lake lilikuwa vilima vya milele. Mtoa-Sheria wa Kiungu alishuka juu ya mlima wenye miamba ili kunena sheria Yake masikioni mwa watu wote, ili ukuu na utisho wa udhihirisho wa nguvu na utukufu Wake uwaguse kwa kina, na waogope kuzivunja amri Zake. Mungu alinena sheria Yake katikati ya ngurumo na miale

ya umeme na lile wingu zito lililokuwa juu ya kilele cha mlima, na sauti Yake ilikuwa kama sauti ya tarumbeta iliyolia kwa nguvu sana. Sheria ya Yehova haikubadilika, na mbao ambazo aliandika juu yake sheria hiyo zilikuwa za mwamba imara, zikimaanisha kutobadilika kwa maagizo Yake. Horebu yenye miamba ikawa mahali Patakatifu kwa wote waliopenda na kuiheshimu sheria ya Mungu. **{SLsw 74.3}**

Akiwa Katika Ushirika wa Karibu na Mungu

Yohana alipokuwa akitafakari mandhari ya Horebu/Sinai, Roho wa Yeye aliyeitakasa siku ya saba alikuja juu yake. Alitafakari juu ya dhambi ya Adamu katika kuivunja sheria ya Mungu, pamoja na matokeo ya kutisha ya uasi huo. Upendo usio na kikomo wa Mungu, katika kumtoa Mwana Wake ili kukomboa jamii ya mwanadamu iliyopotea, ulionekana kuwa mkuu mno kiasi cha kutoweza kuelezeka kwa maneno. Anapoeleza upendo huo katika waraka wake, analiita kanisa na ulimwengu kuutazama. ***"Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hiyo ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua Yeye"*** (1 Yohana 3:1). Kwa Yohana ilikuwa fumbo kwamba

Mungu angeweza kumtoa Mwana Wake afe kwa ajili ya mwanadamu mwasi. Naye alijawa na mshangao mkuu alipotafakari kwamba mpango wa wokovu, uliobuniwa kwa gharama kubwa sana mbele za Mbingu, ungekatalaliwa na wale ambao kwa ajili yao dhabihu hiyo isiyo na kikomo ilitolewa. **{SL 75.1}**

Yohana alikuwa amejitenga na mambo mengine na kuwa katika ushirika wa karibu na Mungu-amejifungia ili kuwa na Mungu tu! Alipojifunza zaidi kuhusu tabia ya Mungu kupitia kazi za uumbaji, heshima yake kwa Mungu ilizidi kuongezeka. Mara nyingi alijiuliza, **"Kwa nini wanadamu, ambao wanamtegemea Mungu kabisa, wasitafute kuwa na amani Naye kwa kumtii kwa hiari?"** Ana hekima isiyo na kikomo, wala hakuna mpaka wa nguvu Zake. Anazitawala mbingu pamoja na ulimwengu usiohesabika uliomo humo. Anahifadhi kwa upatanifu mkamilifu ukuu na uzuri wa vitu alivyoviumba. Dhambi ni uasi dhidi ya sheria ya Mungu, na mshahara wa dhambi ni mauti. Kusingekuwa na mifarakano mbinguni wala duniani ikiwa dhambi isingeingia. Kutotii sheria ya Mungu kumeleta taabu zote zilizowahi kuwapo miongoni mwa viumbe Vyake. Kwa nini wanadamu hawataki kupatanishwa na Mungu? **{SLsw 75.2}**

Si jambo dogo kumtenda Mungu dhambi, au kuuweka utashi mpotovu wa mwanadamu kinyume na mapenzi ya Muumba wake. Ni kwa manufaa ya mwanadamu makubwa, hata katika ulimwengu huu, kwamba wanadamu wayatii maagizo ya Mungu. Na kwa hakika ni kwa manufaa yao ya milele kujisalimisha kwa Mungu na kuwa na amani Naye. Wanyama wa kondeni hutii sheria ya Muumba wao kupitia silika inayowaongoza. Yeye huiambia bahari yenye kiburi, ***"Utafika mpaka hapa, wala hutapita"*** (Ayubu 38:11); nayo maji hutii Neno Lake mara moja. Sayari zimepangwa kwa utaratibu mkamilifu, zikitii sheria ambazo Mungu ameziweka. Katika viumbe vyote ambavyo Mungu ameviumba duniani, mwanadamu peke yake ndiye aliye mwasi. Hata hivyo, amepewa uwezo wa kufikiri ili kuelewa madai ya sheria ya Mungu, pamoja na dhamiri inayoweza kuhisi hatia ya uasi, na pia amani na furaha vinavyotokana na utii. Mungu alimfanya kuwa kiumbe mwenye uhuru wa kimaadili, aweze kuchagua kutii au kutotii. Thawabu ya uzima wa milele—utukufu wa milele usio na kifani—imeahidiwa kwa wale wanaofanya mapenzi ya Mungu, huku vitisho vya ghadhabu Yake vikining'inia juu ya wote wanaokaidi sheria Yake. **{SLsw 76.1}**

Ukuu wa Mungu

Yohana alipokuwa akitafakari utukufu wa Mungu uliofunuliwa katika kazi Zake, alijawa na mshangao mbele ya ukuu na adhama ya Muumba. Endapo wakazi wote wa ulimwengu huu mdogo wangekataa kumtii Mungu, Yeye hangekosa utukufu-hangeachwa bila utukufu. Yeye Angeweza kuwafagilia mbali wanadamu wote duniani kwa muda mfupi na kuumba kizazi kipya cha wanadamu ili kuijaza dunia hii na kulitukuza jina Lake. Mungu hamtegemei mwanadamu ili apate heshima. Angeweza kuyapanga majeshi ya nyota za mbinguni na mamilioni ya ulimwengu ulio juu ili yainue wimbo wa heshima, sifa, na utukufu kwa Muumba wao. ***"Ee Bwana, mbingu zitayasifu maajabu Yako, Uaminifu Wako katika kusanyiko la watakatifu. Maana ni nani katika mbingu awezaye kulinganishwa na Bwana? Ni nani afananaye na Bwana miongoni mwa malaika? Mungu huogopwa sana barazani pa watakatifu, Ni wa kuhofiwa kuliko wote wanaomzunguka."*** (Zaburi 89:5–7). **{SLsw 76.2}**

Maono ya Kristo

Yohana anakumbuka matukio ya ajabu aliyoshuhudia katika maisha ya Kristo. Katika mawazo yake, anafurahia tena fursa hizo za thamani ambazo hapo awali alibarikiwa kuwa nazo, naye anapata faraja kubwa. Ghafla, tafakari yake inakatizwa; anaitwa kwa sauti iliyo wazi na bainifu. Anageuka ili kuona sauti hiyo inatoka wapi, na tazama! Anamwona Bwana wake, ambaye amempenda, ambaye ametembea na kuzungumza naye, na ambaye ameshuhudia mateso Yake msalabani. Lakini jinsi sura ya Mwokozi ilivyobadilika! Yeye si tena ***"mtu wa huzuni, ajuaye sikitiko"*** (Isaya 53:3). Hakuwa tena na alama za kudhalilishwa Kwake. Macho Yake ni kama mwali wa moto; miguu Yake ni kama shaba safi inayong'aa katika tanuru. Sauti Yake inasikika kama mvumo wa maji mengi. Uso Wake unang'aa kama jua katika utukufu wake wa adhuhuri. Mkono Wake ulikuwa na nyota saba, zinazowakilisha wahudumu wa makanisa. Kinywani Mwake ulitoka upanga mkali wenye makali kuwili, ukiwa ishara ya nguvu ya Neno Lake. **{SLsw 77.1}**

Yohana, ambaye amempenda sana Bwana wake na ambaye ameshikamana kwa uthabiti na Kweli mbele ya vifungo, mapigo, na tishio la kifo, hawezi kustahimili utukufu mkuu wa uwepo wa Kristo, naye anaanguka chini kama mtu aliyepigwa na mauti. Ndipo Yesu anaweka

mkono Wake juu ya mtumishi Wake aliyeanguka, akisema, ***"Usiogope; ... Mimi Ndiye Aliye hai, Nami nalikuwa nimekufa; na tazama, ni hai hata milele na milele"*** (Ufunuo 1:17, 18). Yohana anatiwa nguvu ili aweze kuishi mbele ya Bwana wake aliyetukuzwa, na kisha, katika maono matakatifu, akaonyeshwa makusudi ya Mungu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Uzuri na utukufu wa makao ya mbinguni ulifunuliwa kwake. Aliruhusiwa kukitazama kiti cha enzi cha Mungu na kuuuona umati wa waliokombolewa wakiwa wamevaa mavazi meupe. Alisikia muziki wa malaika wa mbinguni na nyimbo za ushindi kutoka kwa wale walioshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa neno la ushuhuda wao. **{SLsw 78.1}**

Unyenyekevu wa Yohana

Mwanafunzi huyo mpendwa alipewa fursa tukufu ambazo ni nadra sana kutunukiwa wanadamu. Hata hivyo, kwa kuwa alikuwa amefanana kwa karibu sana na tabia ya Kristo, kiburi hakikupata nafasi moyoni mwake. Unyenyekevu wake haukuwa jambo la kujionyesha kwa maneno ya mdomo tu; ulikuwa neema iliyomvaa kwa kawaida kama vazi. Daima alijitahidi kuficha matendo yake mwenyewe ya haki na kuepuka jambo lolote ambalo

lingeonekana kuvuta fikira za watu kwake. Katika Injili yake, Yohana anamtaja mwanafunzi ambaye Yesu alimpenda, lakini anaficha ukweli kwamba mwanafunzi huyo aliyependwa na kuheshimiwa alikuwa yeye mwenyewe. Maisha yake hayakuwa na ubinafsi. Katika maisha yake ya kila siku, alifundisha na kuutenda upendo kwa maana yake kamili. Alikuwa na uelewa wa kina kuhusu upendo unaopaswa kuwepo kati ya ndugu wa damu na ndugu katika Kristo. Anaueleza na kuuhimiza upendo huu kuwa sifa ya msingi ya wafuasi wa Yesu. Bila upendo huo, madai yote ya kuitwa Mkristo hayana maana. **{SLsw 78.2}**

Yohana alikuwa mwalimu wa utakatifu unaodhihirika katika maisha. Aliweka kanuni sahihi na zisizopotosha za mwenendo wa Kikristo. Wakristo wanapaswa kuwa safi moyoni na wenye mwenendo unaofaa. Katika hali yoyote hawapaswi kuridhika na ukiri wa imani usio na matendo. Anaeleza kwa maneno yaliyo wazi kabisa kwamba kuwa Mkristo ni kuwa kama Kristo. **{SLsw 79.1}**

Maisha ya Yohana yalikuwa ya juhudi ya dhati ya kuishi kulingana na mapenzi ya Mungu. Mtume alimfuata Mwokozi wake kwa ukaribu sana, na alikuwa ametambua kwa kina sana usafi na utakatifu mkuu wa Kristo, kiasi

kwamba tabia yake mwenyewe ilionekana kuwa yenye upungufu mkubwa ilipolinganishwa na ya Kristo. Yesu alipomtokea Yohana katika mwili Wake uliotukuzwa, kumtazama mara moja tu kulitosha kumfanya aanguke chini kama mtu aliyekufa. Hivyo ndivyo wale wanaomjua vizuri zaidi Bwana na Mwalimu wao wanavyohisi daima. Kadiri wanavyotafakari kwa ukaribu zaidi maisha na tabia ya Yesu, ndivyo wanavyohisi kwa undani zaidi hali yao wenyewe ya dhambi, na ndivyo wanavyokuwa na mwelekeo mdogo zaidi wa kudai kuwa wana utakatifu wa moyo au kujisifu kwa utakaso wao. **{SLsw 79.2}**

SURA YA 10—TABIA YA KIKRISTO

Tabia ya Mkristo huonekana katika maisha yake ya kila siku. Kristo alisema, ***"Kila mti mwema huzaa matunda mazuri; bali mti mwovu huzaa matunda mabaya"*** (Mathayo 7:17). Mwokozi wetu anajilinganisha na mzabibu, ambao wafuasi Wake ni matawi yake. Anaeleza wazi kwamba wote wanaotaka kuwa wanafunzi Wake lazima wazae matunda; kisha anaonyesha jinsi wanavyoweza kuwa matawi yenye kuzaa matunda.

"Kaeni ndani Yangu, Nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani Yangu." (Yohana 15:4). **{SLsw 80.1}**

Mtume Paulo anaeleza matunda ambayo Mkristo anapaswa kuzaa. Anasema kwamba matunda hayo ***"huonekana katika wema wote na haki na Kweli"*** (Waefeso 5:9). Tena anasema, ***"Tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, wema, imani, upole, kiasi"*** (Wagalatia 5:22, 23). Neema hizi za thamani ni kanuni za sheria ya Mungu zinazotimizwa katika maisha. **{SLsw 80.2}**

Sheria ya Mungu ndiyo kiwango pekee cha Kweli cha ukamilifu wa maadili. Sheria hiyo ilidhihirishwa kwa vitendo katika maisha ya Kristo. Yeye Mwenyewe anasema, ***"Nimezishika amri za Baba Yangu"*** (Yohana 15:10). Hakuna utii ulio chini ya huu unaoweza kukidhi matakwa ya Neno la Mungu. ***"Yeye asemaye kwamba anakaa ndani Yake, imempasa kuenenda mwenyewe vilevile kama Yeye alivyoenenda"*** (1 Yohana 2:6). Hatuwezi kutoa udhuru kwamba hatuwezi kufanya hivyo, kwa maana tumepewa ahadi hii: ***"Neema Yangu yakutosha"*** (2 Wakorintho 12:9). Tunapotazama katika

kioo cha Mungu, yaani, sheria Yake, tunaona ubaya mkubwa mno wa dhambi na hali yetu wenyewe ya kupotea kama wavunjaji wa sheria. Lakini kwa njia ya toba na imani tunahesabiwa haki mbele za Mungu, na kwa neema ya Mungu tunawezeshwa kumtii na kuzishika amri Zake. **{SLsw 80.3}**

Upendo kwa Mungu na Mwanadamu

Wale walio na upendo wa Kweli kwa Mungu wataonyesha shauku ya dhati ya kujua mapenzi Yake na kuyatenda. Mtume Yohana, ambaye nyaraka zake zinaeleza kwa kina sana kuhusu upendo, anasema, ***"Huku ndiko kumpenda Mungu: kwamba tuzishike amri Zake"*** (1 Yohana 5:3). Mtoto anayewapenda wazazi wake ataonyesha upendo huo kwa utii wa hiari; lakini mtoto mwenye ubinafsi na asiye na shukrani hujitahidi kufanya machache kadri iwezekanavyo kwa ajili ya wazazi wake, huku wakati huohuo akitaka kufurahia fursa (upendeleo) zote wanazopewa watoto watiifu na waaminifu. Tofauti hiyo hiyo inaonekana miongoni mwa wale wanaodai kuwa watoto wa Mungu. Wengi wanaojua kwamba ni watu wanaopendwa na kutunzwa na Mungu, na wanaotamani kupokea baraka Zake, hawafurahii kutenda mapenzi Yake. Wanayaona madai ya Mungu kwao kuwa

kizuizi kisichopendeza, na amri Zake kuwa nira yenye kulemea. Lakini mtu anayetamani kwa kweli utakatifu wa moyo na wa maisha hufurahia sheria ya Mungu, na huomboleza kwa sababu tu anajiona kuwa amepungukiwa sana katika kutimiza matakwa yake. **{SLsw 81.1}**

Tumeamriwa kupendana kama Kristo alivyotupenda. Yeye Ameudhihirisha upendo Wake kwa kutoa maisha Yake ili atukomboe. Mwanafunzi huyo mpendwa anasema kwamba tunapaswa kuwa tayari kuutoa uhai wetu kwa ajili ya ndugu. Kwa maana ***"Kila mtu ampendaye mwenye kuzaa, ampenda hata yeye aliyezaliwa na Yeye."*** (mstari wa 1). Ikiwa tunampenda Kristo, tutawapenda wale wanaofanana Naye katika maisha na katika tabia. Na si hivyo tu, bali tutawapenda pia wale ambao ***"hawakuwa na tumaini,"*** na ambao walikuwa ***"hawana Mungu duniani"*** (Waefeso 2:12). Ilikuwa kwa ajili ya kuwaokoa wenye dhambi kwamba Kristo aliacha makao Yake ya mbinguni na kuja duniani kuteseka na kufa. Kwa ajili hiyo alihenyeka na kazi kwa bidii, akahangaika na kuomba, mpaka, akiwa amevunjika moyo na kuachwa na wale aliokuja kuwaokoa, akautoa uhai Wake pale Kalvari. **{SLsw 82.1}**

Kuiga Kielelezo

Wengi husita kuishi maisha kama yale ambayo Mwokozi wetu aliishi. Wanaona kwamba kuiga Kielelezo, kuzaa matunda ya matendo mema, na kisha kustahimili kwa saburi kusafishwa/kupogolewa na Mungu ili waweze kuzaa matunda zaidi, kunahitaji kujitoa mhanga kupita kiasi. Lakini Mkristo anapojiona kuwa chombo duni tu mikononi mwa Kristo na kujitahidi kutimiza kwa uaminifu kila wajibu, akitegemea msaada ambao Mungu ameahidi, huvaa nira ya Kristo na kuiona kuwa ni rahisi; hubeba mizigo kwa ajili ya Kristo na kuitambua kuwa ni myepesi. Anaweza kuinua macho yake kwa ujasiri na kwa tumaini, na kusema, ***"Namjua Yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana Kwake"*** (2 Timotheo 1:12). **{SLsw 82.2}**

Tukikutana na vikwazo katika njia yetu na kuvishinda kwa uaminifu; tukikabili upinzani na lawama na, kwa Jina la Kristo, tukapata ushindi; tukibeba majukumu na kutimiza wajibu wetu katika roho ya Bwana wetu—hapo ndipo, kwa hakika, tunapopata ujuzi wa thamani kuhusu uaminifu Wake na nguvu Zake. Hatuutegemei tena uzoefu wa wengine, kwa maana tunao ushuhuda ndani yetu wenyewe. Kama Wasamaria wa zamani, tunaweza kusema, ***"maana sisi tumesikia***

wenyewe, tena twajua ya kuwa hakika Huyu Ndiye Mwokozi wa ulimwengu." (Yohana 4:42). **{SLsw 83.1}**

Kadiri tunavyotafakari zaidi tabia ya Kristo, na kadiri tunavyopitia zaidi nguvu Yake ya kuokoa maishani mwetu, ndivyo tutakavyotambua kwa undani zaidi udhaifu na hali yetu ya kutokamilika, na ndivyo tutakavyomtegemea kwa bidii zaidi kuwa nguvu yetu na Mkombozi wetu. Hatuna nguvu ndani yetu wenyewe ya kulitakasa hekalu la nafsi kutokana na unajisi wake; lakini tunapotubu dhambi zetu dhidi ya Mungu na kutafuta msamaha kwa msingi wa ustahili wa Kristo, Yeye atatupatia ile imani itendayo kazi kwa upendo na kuutakasa moyo. Kwa imani katika Kristo na kwa utii kwa sheria ya Mungu, tunaweza kutakaswa, na hivyo kufanywa wenye kufaa kwa ajili ya ushirika wa malaika watakatifu pamoja na waliokombolewa waliovaa mavazi meupe katika ufalme wa utukufu. **{SLsw 83.2}**

Umoja na Kristo—Upendeleo Wetu

Si upendeleo tu, bali pia ni wajibu wa kila Mkristo kudumisha umoja wa karibu na Kristo na kuwa na uzoefu wa kina katika mambo ya Mungu. Ndipo maisha yake yatazaa matunda ya matendo mema. Kristo alisema, ***"Hivyo hutukuzwa Baba Yangu, kwa vile mzaavyo***

sana.” (Yohana 15:8). Tunaposoma maisha ya watu waliokuwa mashuhuri kwa utauwa wao, mara nyingi tunaona uzoefu wao wa kiroho na mafanikio yao kuwa ni mambo yaliyo mbali sana na uwezo wetu. Lakini sivyo ilivyo. Kristo alikufa kwa ajili ya wote; na tunahakikishiwa katika Neno Lake kwamba Yeye Yuko tayari sana kuwapa Roho Wake Mtakatifu wale wanaomwomba kuliko wazazi wa kibinadamu walivyo tayari kuwapa watoto wao vipawa vyema. Manabii na mitume hawakufikia ukamilifu wa tabia ya Kikristo kwa muujiza. Walitumia njia ambazo Mungu alikuwa ameziweka katika uwezo wao; na wote watakaowekeza juhudi kama hizo watapata matokeo kama hayo. **{SLsw 83.3}**

Maombi ya Paulo kwa Ajili ya Kanisa

Katika barua yake kwa kanisa la Efeso, Paulo anaweka mbele yao ***“siri ya Injili”*** (Waefeso 6:19), ***“utajiri wake Kristo usiopimika”*** (Waefeso 3:8), kisha anawahakikishia kuhusu maombi yake ya dhati na bidii kwa ajili ya ustawi wao wa kiroho: **{SLsw 84.1}**

“Kwa hiyo nampigia Baba magoti, ambaye kwa Jina Lake Ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa, awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu Wake,

kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho Wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu." (Waefeso 3:14–19). **{SLsw 84.2}**

Anawaandikia pia ndugu zake wa Korintho, ***"waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu, pamoja na wote wanaoliitia Jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu. Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwa Mungu Baba yetu, na kwa Bwana Yesu Kristo. Namshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, kwa sababu ya neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo Yesu; kwa kuwa katika kila jambo mlitajirika katika Yeye, katika maneno yote, na maarifa yote; kama ushuhuda wa Kristo ulivyothibitika kwenu; hata hamkupungukiwa na karama yo yote, mkikutazamia sana kufunuliwa Kwake Bwana wetu Yesu Kristo;"*** (1 Wakorintho 1:2–7). Maneno haya hayakuelekezwa na kutamkwa kwa kanisa la Korintho pekee, bali pia kwa watu wote wa Mungu

mpaka mwisho wa wakati. Kila Mkristo anaweza kufurahia baraka ya utakaso. **{SLsw 84.3}**

Mtume anaendelea kwa maneno haya: ***"Basi ndugu, nawasihi, kwa Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja."*** (mstari wa 10). Paulo asingewasihi wafanye jambo lisilowezekana. Umoja ni matokeo ya hakika ya ukamilifu wa Kikristo. **{SLsw 85.1}**

Katika Waraka kwa Wakolosai pia kunaelezwa fursa tukufu walizopewa watoto wa Mungu. ***"tangu tuliposikia habari za imani yenu katika Kristo Yesu, na upendo mlio nao kwa watakatifu wote… sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi Yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu; mkiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha"*** (Wakolosai 1:4–11). **{SLsw 85.2}**

Kiwango cha Utakatifu

Mtume mwenyewe alikuwa akijitahidi kufikia kiwango hicho cha utakatifu alichokiweka mbele ya ndugu zake. Anawaandikia Wafilipi: ***"Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu…. ili nimjue Yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso Yake, nikifananishwa na kufa Kwake; ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiyama ya wafu. Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu."*** (Wafilipi 3:7–14). **{SLsw 87.1}**

Mapenzi ya Mungu

Paulo hakusita kusisitiza, kila alipopata nafasi inayofaa, umuhimu wa utakaso wa Kibiblia. Anasema: ***"Mnajua ni maagizo gani tuliwapa kwa Bwana Yesu.***

Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, yaani, kutakaswa kwenu” (1 Wathesalonike 4:2, 3). ***“Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema. Yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano, mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu,”*** (Wafilipi 2:12–15). **{SLsw 86.2}**

Anamwagiza Tito awafundishe waumini kwamba, ingawa wanapaswa kutegemea sifa na Stahiki za Kristo kwa ajili ya wokovu, neema ya Mungu inapokaa mioyoni mwao itawaongoza kutimiza kwa uaminifu wajibu wote wa maisha. **“*Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari kwa kila kazi njema; wasimtukane mtu yeyote, wasiwe wagomvi, wawe wema, wakionyesha upole wote kwa watu wote. Maana hapo zamani sisi nasi tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi, tumedanganywa, huku***

tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda, tukichukiza na kuchukiana. Lakini wema Wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo Wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema Yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu; ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu; ili tukihesabiwa haki kwa neema Yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu. Ni Neno la kuaminiwa; na mambo hayo nataka uyanene kwa nguvu, ili wale waliomwamini Mungu wakumbuke kudumu katika matendo mema. Hayo ni mazuri, tena yana faida kwa wanadamu." (Tito 3:1–8). **{SLsw 87.1}**

Paulo anataka kutia akilini mwetu Ukweli kwamba msingi wa utumishi wote unaokubalika mbele za Mungu, pamoja na kilele cha fadhila za Kikristo, ni upendo; na kwamba amani ya Mungu itakaa tu katika nafsi ambayo upendo unatawala. ***"Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe***

ninyi, vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu. Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani. Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa Yeye." (Wakolosai 3:12–17). **{SLsw 87.2}**

SURA YA 11—UPENDELEO WA MKRISTO

Wengi wanaotafuta kwa unyoofu utakatifu wa moyo na usafi wa maisha huonekana kukanganyikiwa na kukata tamaa. Daima hujitazama wenyewe na kulalamika kwa sababu ya ukosefu wao wa imani; na kwa kuwa hawahisi kuwa wana imani, wanaona kwamba hawawezi kudai

baraka ya Mungu. Watu hawa wanachanganya hisia na imani. Wanatafuta jambo lililo juu ya usahili wa imani ya Kweli, na kwa kufanya hivyo huleta giza kubwa juu ya nafsi zao. Wanapaswa kuielekeza akili yao mbali na nafsi zao na kuitafakari rehema na wema wa Mungu, wakikumbuka ahadi Zake; kisha waamini tu kwamba Yeye atatimiza Neno Lake. **Hatupaswi kutegemea imani yetu, bali kutegemea ahadi za Mungu.** Tunapotubu makosa yetu ya zamani dhidi ya sheria Yake na kuazimia kutii katika siku zijazo, tunapaswa kuamini kwamba Mungu, kwa ajili ya Kristo, anatupokea na kutusamehe dhambi zetu. **{SLsw 89.1}**

Nyakati fulani giza na kukata tamaa huja juu ya nafsi na kutishia kutushinda, lakini hatupaswi kuitupilia mbali imani yetu. Ni lazima tumtazame Yesu daima, iwe tunahisi au hatuhisi chochote. Tunapaswa kujitahidi kutimiza kwa uaminifu kila wajibu tunaotambua kuwa ni wetu, kisha tupumzike kwa utulivu katika ahadi za Mungu. **{SLsw 89.2}**

Maisha ya Imani

Nyakati fulani, hisia ya kina ya kutostahili kwetu inaweza kuleta mshtuko wa hofu ndani ya nafsi; lakini jambo hili si ushahidi kwamba Mungu amebadilika katika

mtazamo Wake kwetu, wala kwamba sisi tumebadilika katika uhusiano wetu na Mungu. Hatupaswi kujilazimisha kufikia kiwango fulani cha hisia. Huenda leo tusihisi amani na furaha tulizohisi jana; lakini kwa imani tunapaswa kuushika mkono wa Kristo na kumtumaini kikamilifu katika giza kama tunavyomtumaini katika nuru. **{SLsw 90.1}**

Shetani anaweza kunong'ona, "Wewe ni mwenye dhambi nyingi mno kiasi kwamba Kristo hawezi kukuokoa." Ingawa unakiri kwamba kwa hakika wewe ni mwenye dhambi na hustahili chochote chema kwa nguvu zako mwenyewe, wewe unaweza kumjibu yule mjaribu kwa kusema kwa uthabiti, "Kwa msingi wa upatanisho, ninamshikilia Kristo kuwa Mwokozi wangu. Sijitumaini katika ustahili wangu mwenyewe, bali katika damu ya thamani ya Yesu, inayotakasa. Wakati huu naiweka nafsi yangu isiyojiweza mikononi mwa Kristo." Maisha ya Kikristo yanapaswa kuwa maisha ya imani ya endelevu, inayodumu na iliyo hai. Kumtumaini Kristo bila kuyumba na kumtegemea kwa uthabiti kutaleta amani na hakikisho moyoni. **{SLsw 90.2}**

Kushinda Vishawishi

Usikate tamaa kwa sababu moyo wako unaonekana kuwa mgumu. Kila kizuizi na kila adui wa ndani hufanya hitaji lako la Kristo kuwa kubwa zaidi. Yeye Alikuja kuuondoa moyo wa jiwe kwako na kukupa moyo wa nyama. Mtazame Yeye ili akupe neema ya pekee ya kushinda udhaifu wako wa pekee. Unaposhambuliwa na jaribu, pinga kwa uthabiti misukumo hiyo mibaya; iambie nafsi yako, “Ninawezaje kumvunjia heshima Mkombozi wangu? Nimejitoa kwa Kristo; mimi siwezi kufanya matendo ya Shetani.” Mlilie Mwokozi mpendwa akupe msaada wa kuondoa kila sanamu na kuacha kila dhambi ambayo ni kipenzi chako [darling sin]. Jicho la imani na limwone Yesu akiwa amesimama mbele ya kiti cha enzi cha Baba, akionyesha mikono Yake iliyojeruhiwa huku akikuombea. Amini kwamba nguvu inakuja kwako kupitia Mwokozi wako wa thamani. **{SLsw 90.3}**

Kutazama kwa Jicho la Imani

Kwa imani, zitazame taji zilizowekwa tayari kwa ajili ya wale watakaoshinda; sikiliza wimbo wa shangwe wa waliokombolewa: “Astahili, astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, Naye ametukomboa kwa ajili ya Mungu!” Jitahidi kuyatazama matukio hayo kana kwamba ni halisi. Stefano, shahidi wa kwanza wa Kikristo, katika pambano

lake la kutisha dhidi ya falme na mamlaka na nguvu za uovu wa rohoni katika ulimwengu wa juu, alipaza sauti akisema, ***"Akasema, Tazama! Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu."*** (Matendo 7:56). Mwokozi wa ulimwengu alifunuliwa kwake, akiwa anamwangalia kutoka mbinguni kwa shauku kuu, na nuru tukufu ya uso wa Kristo ilimwangazia Stefano kwa uangavu mkubwa kiasi kwamba hata maadui zake waliona uso wake uking'aa kama uso wa malaika. **{SLsw 91.1}**

Ikiwa tungeliruhusu akili zetu zitafakari zaidi juu ya Kristo na ulimwengu wa mbinguni, tungepata kichocheo chenye nguvu na msaada katika kupigana vita vya Bwana. Kiburi na upendo wa ulimwengu vitapoteza nguvu zake tunapotafakari utukufu wa nchi ile bora, ambayo hivi karibuni itakuwa makao yetu. Kwa kulinganisha na uzuri wa Kristo, mvuto wote wa dunia utaonekana kuwa wa thamani ndogo. **{SLsw 91.2}**

Mtu yeyote asidhani kwamba anaweza kupata hakikisho la upendo wa Mungu bila kufanya juhudi ya dhati kwa upande wake. Akili inapokuwa imeruhusiwa kwa muda mrefu kutafakari mambo ya kidunia pekee, si jambo rahisi kubadili mazoea ya kufikiri. Yale ambayo

jicho huona na sikio husikia mara nyingi huvutia fikira na kuteka uangalifu. Lakini ikiwa tunataka kuingia katika mji wa Mungu na kumtazama Yesu pamoja na utukufu Wake, lazima tuzoee kumtazama kwa jicho la imani tukiwa hapa duniani. Maneno na tabia ya Kristo vinapaswa kuwa jambo la mara kwa mara katika mawazo na mazungumzo yetu, na kila siku tunapaswa kutenga muda maalumu kwa ajili ya kutafakari kwa maombi mambo haya matakatifu. **{SLsw 91.3}**

Kunyamazisha Sauti ya Roho

Utakaso ni kazi ya kila siku. Mtu yeyote asijidanganye kwa kuamini kwamba Mungu atamsamehe na kumbariki huku akiendelea kukanyaga mojawapo ya amri Zake. Kutenda kwa makusudi dhambi ambayo mtu anajua kuwa ni dhambi hunyamazisha sauti ya Roho inayoshuhudia ndani yake na kuitenga nafsi yake na Mungu. Haidhuru msisimko wa hisia za kidini uwe mkubwa kiasi gani, Yesu hawezi kukaa moyoni mwa mtu anayepuuza sheria ya Mungu. Mungu atawaheshimu wale tu wanaomheshimu Yeye. **{SLsw 92.1}**

"Ninyi ni watumwa wa yule mnayemtii" (Warumi 6:16). Tukijiruhusu kuendekeza na kutawaliwa na hasira, tamaa, uchoyo, chuki, ubinafsi, au dhambi nyingine

yoyote, tunakuwa watumwa wa dhambi. ***"Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili"*** (Mathayo 6:24). Tukitumikia dhambi, hatuwezi kumtumikia Kristo. Mkristo atahisi misukumo ya dhambi, kwa maana mwili hutamani kinyume cha Roho; lakini Roho hupigana na mwili, na hivyo kudumisha pambano la daima. Hapa ndipo msaada wa Kristo unapohitajika. Udhaifu wa kibinadamu huunganishwa na nguvu ya Mungu, na imani hupaza sauti ikisema, ***"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo."*** (1 Wakorintho 15:57)! **{SLsw 92.2}**

Mazoea Sahihi ya Kidini

Ili tuweze kujenga tabia inayokubalika mbele za Mungu, ni lazima tujenge mazoea sahihi katika maisha yetu ya kidini. Maombi ya kila siku ni muhimu kwa ukuaji katika neema, na hata kwa maisha ya kiroho yenyewe, kama vile chakula cha kimwili kilivyo muhimu kwa ustawi wa mwili. Tunapaswa kujizoeza kuyainua mawazo yetu mara kwa mara kwa Mungu katika maombi. Mawazo yetu yanapotangatanga, ni lazima tuyarejeshe; kwa juhudi ya kudumu, hatimaye mazoea yatafanya jambo hilo kuwa rahisi. Hatuwezi kujitenga na Kristo hata kwa muda mfupi bila kuhatarisha usalama wetu. Uwepo

Wake unaweza kuandamana nasi katika kila hatua, lakini hilo linawezekana tu kwa kutimiza masharti ambayo Yeye Mwenyewe ameweka. **{SLsw 93.1}**

Dini inapaswa kuwa jambo kuu la maisha-biashara kuu ya maisha! Mambo mengine yote yanapaswa kuwa chini ya jambo hili. Nguvu zetu zote—za nafsi, mwili, na roho—lazima zihusishwe katika pambano la Kikristo. Ni lazima tumtazame Kristo kwa ajili ya nguvu na neema, nasi tutapata ushindi kwa hakika kama vile Yesu alivyokufa kwa ajili yetu. **{SLsw 93.2}**

Thamani ya Nafsi

Tunapaswa kusogea karibu zaidi na msalaba wa Kristo. Toba chini ya msalaba ndiyo somo la kwanza la amani tunalopaswa kujifunza. Upendo wa Yesu—Je, ni nani awezaye kuuelewa? Ni mpole na wa kujikana nafsi kuliko hata upendo wa mama! Ikiwa tunataka kujua thamani ya nafsi ya mwanadamu, ni lazima kwa imani hai tutazame msalaba, na hivyo kuanza kujifunza somo ambalo litakuwa sayansi na wimbo wa waliokombolewa milele yote. Thamani ya wakati na vipawa vyetu inaweza kukadiriwa tu kwa kuzingatia ukuu wa fidia iliyolipwa kwa ajili ya ukombozi wetu. Ni ukosefu mkubwa wa shukrani ulioje, tunaomdhihirishia Mungu tunapomnyima

vilivyo Vyake kwa kumnyima upendo wetu na utumishi wetu! Je, ni jambo kubwa mno kujitoa wenyewe kwa Yeye ambaye alijitoa mhanga kabisa kwa ajili yetu? Je, tunaweza kuchagua urafiki wa ulimwengu badala ya heshima za milele ambazo Kristo anatupatia—***"Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja Nami katika kiti changu cha enzi, kama Mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba Yangu katika kiti chake cha enzi."*** (Ufunuo 3:21)? **{SLsw 93.3}**

Kazi ya Hatua kwa Hatua

Utakaso ni kazi ya hatua kwa hatua. Hatua zinazofuatana zimewekwa wazi katika maneno ya Petro: ***"Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo."*** (2 Petro 1:5–8). ***"Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo***

hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo." (mstari wa 10, 11). **{SLsw 94.1}**

Hii ndiyo njia ambayo kupitia hiyo tunaweza kuwa na hakika kwamba hatutaanguka kamwe. Wale wanaojenga sifa za Kikristo kwa kufuata mpango huu wa kuongeza+, sifa moja baada ya nyingine wana hakikisho kwamba Mungu atafanya kazi kwa mpango wa kuzidisha katika kuwajalia karama za Roho Wake. Petro anawaandikia wale waliopokea imani yenye thamani kama ile tuliyo nayo: ***"Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu."*** (mstari wa 2). Kwa neema ya Mungu, wote walio tayari wanaweza kupanda hatua hizo zenye kung'aa kutoka duniani kwenda mbinguni, na hatimaye, ***"kwa nyimbo na furaha ya milele"*** (Isaya 35:10), kuingia kupitia malango ya jiji la Mungu. **{SLsw 94.2}**

Mwokozi wetu anadai kila kitu tulicho nacho; Yeye Anataka mawazo yetu ya kwanza na matakatifu zaidi, pamoja na upendo wetu wa dhati na wenye nguvu zaidi. Ikiwa kwa kweli tunashiriki katika asili ya Mungu, sifa Zake zitaendelea kuwa mioyoni mwetu na midomoni mwetu. Usalama wetu pekee ni kujisalimisha kikamilifu Kwake na kuendelea kukua katika neema na katika maarifa ya Kweli. **{SLsw 95.1}**

Kilio cha Ushindi cha Paulo

Mtume Paulo aliheshimiwa sana na Mungu, hata akachukuliwa katika maono matakatifu hadi mbingu ya tatu, ambako aliona matukio yenye utukufu ambao hakuruhusiwa kuufunua. Hata hivyo, jambo hilo halikumfanya ajivune wala kujitumaini mwenyewe. Alitambua umuhimu wa kukesha daima na kujikana nafsi, naye anasema waziwazi, ***"bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa."*** (1 Wakorintho 9:27). **{SLsw 95.2}**

Paulo aliteseka kwa ajili ya ile Kweli, lakini hatusikii malalamiko yoyote kutoka midomoni mwake. Anapotazama nyuma katika maisha yake ya taabu, mahangaiko, na kujitoa mhanga, anasema, ***"Kwa maana***

nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu." (Warumi 8:18). Kilio cha ushindi cha mtumishi mwaminifu wa Mungu kinasafiri na kufika mpaka kwenye wakati wetu: ***"Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?..... Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu."*** (Warumi 8:35–39). **{SLsw 95.3}**

Ingawa hatimaye Paulo alifungwa katika gereza la Rumi—akifungiwa mbali na nuru na hewa ya mbinguni, akitengwa na kazi zake za ari na bidii katika Injili, na akitarajia kuhukumiwa kifo wakati wowote—hata hivyo hakujiingiza katika mashaka wala kukata tamaa. Kutoka katika gereza hilo lenye giza kulitoka ushuhuda wake wa mwisho, uliojaa imani kuu na ujasiri ambao umewatia moyo watakatifu na mashahidi katika vizazi vyote vilivyofuata. Maneno yake yanaeleza kwa usahihi

matokeo ya utakaso ambao tumejitahidi kuufafanua katika kurasa hizi: ***"Kwa maana, mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu Mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa Kwake."*** (2 Timotheo 4:6–8). **{SLsw 96.1}**